# WOMEN'S VOICE AND POWER AS AGENTS OF CHANGE

AfWID
AFRICAN WOMEN IN DIALOGUE

Strengthening the Continental African Women's Movement towards a New Value-Based Eco-System




















27 - 31 January 2025 I Birchwood Hotel,
Johannesburg South Africa

WDB | TRUST

# SPONSORS

WDB | TRUST

WIPHOLD

WDB | INVESTMENT HOLDINGS

ARENA HOLDINGS

go2 Travel Alliance
Your one stop travel shop

NELSON MANDELA UNIVERSITY

GENDER LINKS
FOR EQUALITY AND JUSTICE

Telkom

MOTSENG

home affairs
Department:
Home Affairs
REPUBLIC OF SOUTH AFRICA

international relations & cooperation
Department:
International Relations and Cooperation
REPUBLIC OF SOUTH AFRICA

defence
Department:
Defence
REPUBLIC OF SOUTH AFRICA

# UJUMBE KUTOKA KWA MWANZILISHI WETU



## Wanawake Wapendwa Katika Mjadala wa Kiafrika

Wakati wa kifungua kinywa na viongozi wa wanawake, pakiwa na idadi kubwa ya mawaziri, nilikumbuka jinsi, katika tamaduni ya Kiafrika, heshima kawaida hupewa viongozi "mahiri". Katika SAWID, nyakati zote tumechagua kupuuza itifaki za kihierarkia. Tangu mwanzo, tuliamini kwamba sisi sote ni wanawake, na kwa hiyo, tulihitaji kutendea kila mtu katika chumba kwa heshima sawa. Kama matokeo, tulijikuta wakati mwingine tukikaa na Rais katika safu moja, badala ya kumweka mbele, kwani tuliepuka kushiriki katika mvutano wa mamlaka.

Hii ni mara ya tatu sisi ni mwenyeji wa tukio la AfWID. Ulikuwa mpango mdogo sana tulipoanza. Hapo awali, tulikusanyika chumba cha mikutano cha Global Shapers, kikundi cha viongozi wachanga wa Kiafrika waliochaguliwa na Klaus Schwab huko Davos. Mkutano wao ulifanyika katika Southern Sun Hotel, ambapo nilikutana na Bi. Emma Kaliya kutoka Malawi. Wakati wa majadiliano yetu, wazo liliibuka kwamba tunaweza kuleta pamoja wanawake wa SADC kwa ajili ya kuanzisha ajenda yetu wenyewe, badala ya kupitisha tu ajenda za watu wengine. Kwa hakika, programu hizo za nje ni muhimu kwa bara, kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu ya UM na AU Agenda 2063. Hata hivyo, wanawake wa tabaka la chini pia walihitaji kuwa na fursa ya kueleza mambo waliyojionea ili hatua zozote zilizobuniwa ziwe na matokeo chanya.

Katika hoteli hiyo, tulianza kujadili jinsi ya kuwaleta pamoja wanawake wote wa SADC. Hatukujua jinsi jitihada hiyo ingekuwa ghali! Hata hivyo, tangu wakati huo, jitihada zetu zimepanuka ili kuleta bara zima pamoja. Mipango mingi muhimu kwa hatua moja. Siwezi kukumbuka idadi halisi ya washiriki katika mkutano wetu wa kwanza, lakini ulikuwa mkutano wa kawaida uliolenga kuimarisha harakati za wanawake kote Afrika. Lengo lilikuwa kuendeleza miradi yenye ufanisi na kuchukua hatua katika nyanja



WDB | TRUST

muhimu. Njia yetu ilijumuisha mazungumzo ya kikanda ili kutambua masuala muhimu, ambayo yangeelekeza katika mazungumzo makubwa ya bara.

Upatikanaji wa fedha za kutosha kwa hakika ni changamoto kuu. Ingawa tunaweza kujadili jinsi tulivyokusanya pesa zinazohitajika, ninaamini pia kwamba juhudi hizo hazihitaji mikutano ya ana kwa ana kila wakati. Kwa kutumia daftari kidogo, iliyopangwa ambayo kila mshiriki alipokea, tunaweza kukusanya habari za mawasiliano ya kikanda na kuunda mazungumzo ya mtandaoni. Tunapofahamiana, tunaimarisha muungano wetu. Njia hii ya mseto itaturuhusu kudumisha mwendelezo bila kugharimika sana.

Hatua muhimu ya ajenda mwaka huu ni kushughulikia migogoro barani Afrika. Migogoro imeenea sio tu katika bara letu bali ulimwenguni. Siku ya Kwanza tulishuhudia kipindi cha ukimya kwa mshikamano na wanawake walioadhiriwa na mizozo inayoendelea katika nchi thelathini na tano. Lakini zaidi ya ukimya huo, tunawezaje kusaidia?

Katika historia, Mjadala wa Wanawake Wa Afrika Kusini ulihusika kabisa katika utatuzi wa migogoro nchini DRC. Tulialika pande zote Afrika Kusini, tukisisitiza kuwa shida haziwezi kutatuliwa wakati wadau wamegawanyika. Njia yetu ilikuwa kushiriki uzoefu wa Afrika Kusini wa kufanyiza taifa lenye umoja badala ya liligowanyika. Tulihimiza vyama kuanzisha makubaliano ya msingi bila kulazimisha maoni hususa juu yao. Hapo awali, tulipokutana na wanawake, walikuwa na hasira kali na hawakuaminiana, hata walionyesha uadui. Hadithi walizoshiriki zilikuwa masimulizi yenye kuhuzunisha ya ukatili uliofanywa kwa wanawake wajawazito na mateso mengine yasiyowaziwa waliyokuwa wamevumilia.

Walakini, kufikia siku ya tano ya semina, kulikuwa na mabadiliko. Mtaalam wa utatuzi wa migogoro aliongoza zoezi ambalo washiriki waliombwa kuandika matarajio yao kuhusu nchi yao. Walipokuwa wakiripoti, wote walitambua kwamba walikuwa na maono yaleyale. Jambo hilo la lililotuunganisha likawa mwanzo wa upatanisho na ushirikiano.

Kwa kutafakari kuhusu hili, lazima tuzingatie kwa mfano hatua zinazowezekana kwa Msumbiji. Ripoti zinaonyesha kuwa wanasiasa wakuu sasa wako tayari kwa ushirikiano na mazungumzo. Tukiwa wanawake, je tunaweza, kufanikiwa katika hili?

Kuhusiana na DRC, tuliandaa semina iliyojumuisha wawakilishi kutoka kwa uongozi wa jeshi na polisi. Tulisisitiza asilimia 30 ya wanawake wawe katika bunge, lakini wakati mmoja wa Wabunge alipozungumza, alijisisitiza uwakilishi wa 50%— - akizidi pendekezo letu la awali. Hii inaonyesha kuwa hatua zinazolengwa zinaweza kutokeza matokeo muhimu.

Rais Masire alitoa shukrani zake kwa juhudi zetu. Alikuwa ameona mazungumzo ya amani katika Sun City, ambako wanawake awali walijitenga. Hata hivyo, kufuatia ushiriki wetu, wanawake hawa walianza kushirikiana na vyama vyote, kuwezesha mazungumzo na maendeleo.

Tumesikia kutoka kwa wanaharakati wengi na watetezi wa amani wasiotaka kupoteza muda. Hatuwezi kupuuza mizozo inayojitokeza kwenye mipaka yetu. Tulipokea jumbe nyingi za wasiwasi, na kwa wakati mwafaka tukapokea simu kutoka Kwa Phumzile Mlambo Ngcuka, ambaye alipiga tulipokuwa tukijadili hatua za kuchukua. Baadhi ya mapendekezo yalijumuisha kuunda tume ya viongozi wanawake ya kutembelea maeneo yaliyoathiriwa au kuunda nafasi salama sawa na ile tuliyoanzisha kuhusuiana na DRC. Hata hivyo, mpango huo ungehitaji kuratibiwa na wanawake wa eneo hilo ili kuhakikisha kwamba mikutano ina maana inayokusudiwa.

Msumbiji haijawahi kupata demokrasia ya vyama vingi hapo awali. Kubadilisha mfumo kama huo kunahitaji juhudi kubwa, uelewufahamu, na ushirikiano. Mabadiliko ya kisiasa hayafanyiki kwa hiari—yanahitaji mazungumzo yanayoendelea na ushiriki wa kimkakati. Tunapotathmini hali hiyo, lazima tujiulize: ni hatua gani madhubuti tunaweza kuchukua?

Kama wanawake, tuko kwenye njia panda. Ingawa hatuna majibu yote, lazima angalau tuanze mazungumzo. Tunaweza kuungana na kuamua jukumu letu?
Tuko hapa, na lazima tuchukue hatua. Acheni tujadili na tuone jinsi tunaweza kuchangia amani na utulivu katika bara letu.

**Zanele Mbeki, Mwenyekiti WDB Trust na Mwanzilishi wa AfWID**

# KUSHEREHEKEA WANAWAKE KUPITIA DENSI NA IMANI

## NA LEBOGANG MATHEBULA









Mazingira yalikuwa yenye bashaha wanawake kutoka matabaka yote ya maisha walipokuja kujiunga na awamu ya 3 ya Mjadala wa Wanawake wa Kiafrika (AFWID) kwenye Birchwood Hotel mjini Johannesburg. Wajumbe kutoka nchi zote 55 za Afrika walitupamba kwa mitindo ya hali ya juu, rangi na cheche mahiri wakati wa ufunguzi wa shughuli za wiki. Kikundi cha kucheza dansi cha Venda kilianza kwa wimbo na densi zinazosisimua shughuli ya juma hilo.

Makona Zwothe, ambaye inaenzi utamaduni wa Venda kwa kina, alisaidia kuwaingiza washiriki kwenye ukumbi mjadala ulipoanza. Precious Maphakela, ambaye ni kiongozi wa kundi hilo, anasema dhamira yao sio tu kuburudisha tu bali pia kuwaleta wanawake pamoja kupitia sanaa zao. Bila shaka zaidi ya kuwa inavutia, aina yao ya utumbuizaji inatia moyo pia. Wanawake wa kikundi hicho walionyesha kwa shauku kipawa chao kwenye mwingilio wa jumba kuu huku wajumbe wakitambulishwa ngoma na densi zikiendelea. Utendaji huo ulijumuisha roho ya furaha na umoja ambayo inakuwa na watu wa Afrika na kwenye mkutano huu. Moja ya malengo ya mjadala huu ni kufungua nafasi salama, rahisi na yenye furaha kwa wanawake katika bara na kikundi cha densi kiliwakilisha hilo kabisa. Maonyesho hayo hayakuwa tu ya vitumbuizo; yalikuwa sehemu iliyowakilisha mshikamano na tumaini.

Baada ya kumalizika kwa onyesho, washiriki 1000 walielekezwa kwenye ukumbi mkuu ili kuanza rasmi kupitia ibada za imani tofautitofauti. Imphepho (uvumba) ulichomwa ili kuwafariji mababu, na sala zilifanywa na washiriki wa imani za kitamaduni za Kiafrika, Kihindu, Kikristo na Kiislamu. Ibada hizo zilifanywa kwa heshima ya wale wote waliokuwapo katika mkutano huo, kutia ndani nchi zote 55 zilizohudhuria. Sehemu hii ilikuwa msingi katika wiki, iliimarisha wanawake ili baadaye washiriki mapambano wanayokabili katika nchi zao kila siku.

Kwa nyimbo za sauti na sala zenye nguvu za asubuhi, mkutano huo ulikuwa ulianza kwa kishindo, ikionyesha kuwa mkutano wa AFWID 2025 ungethibitika kuwa tukio la mabadiliko na lenye kutokeza kwa wahusika wote.

# ULEMAVU NA UJUMUISHAJI KATIKA AFWID 2025

NA JODI A. LAWRENCE





Ulemavu, na jinsi ya kujumuisha walemavu katika jamii yetu, umekuwa suala nyeti hivi karibuni. Katika mkutano wa mwaka huu wa Afwid 2025, tulikuwa na wajumbe kadhaa kutoka kote Afrika ambao wana ulemavu unaoonekana, na pia wale ambao wana ulemavu ambao hujidhihirisha tu wakati kuna taa kali au sauti kubwa.

Utafiti wa 2021 uliofanywa na Marianne J. W. A Vanderschuren & Obiora A. Nnene unaonyesha kuwa kati ya 10% na 20% ya watu barani Afrika wanaathiriwa na ulemavu. Ukosefu wa ufahamu wa mahitaji na changamoto zinazowakabili walemavu umesababisha kuongezeka kwa kutengwa. Zaidi ya hayo, nchi nyingi barani humu hazijumuishi walemavu inavyofaa katika sheria zao au upangaji miji, na hivyo hufanya iwe vigumu zaidi kwa walemavu kusafiri kwenda kazini, shuleni au hata kwenda burudani. Utafiti huo ulifikia mkataa kwamba usafiri wa walemavu ni wa kiwango cha chini mno kwa kulinganisha na wasio na walemavu.

Ndiyo maana ukumbi wa mkutano wa Afwid 2025 umehakikisha kwamba malazi kadhaa yanafanywa ili kuzingatia changamoto hizi, kama vile njia panda za viti vya magurudumu, viti vya magurudumu na magari ya kusafirisha wajumbe. Rose R. Rapuo, mjumbe Kutoka Kenya, alisema kwamba hakuhisi kutengwa na shughuli zozote ambazo zilifanyika katika kipindi cha siku mbili zilizopita. Rose anatumia mikongojo anapotembea na alisema kuwa njia zilizowekwa katika maeneo yanayofaa katika ukumbi wa mkutano zimefanya ahisi kujumuishwa zaidi.

Hata hivyo, Rose alisema kuwa mambo rahisi kama vile kiti kuwekwa msalani, hayakuzingatiwa, kama ilivyo kwa wengi wetu ambao si kawaida kufikiria changamoto zilw walemavu wanapitia. Ingawa Afwid na hoteli zimehusisha watu wenye ulemavu katika programu mbalimbali na, ni wazi bado kuna uhitaji wa kufanya mipango kwa kushirikisha walemavu.

# KUKABILIANA NA MIGOGORO NA KUPOTEZA MAKAZI

NA HAWA MAYERE

## Eritrea

Eritrea iko kaskazini-mashariki mwa Afrika, kando ya Bahari Nyekundu, inayopakana na Sudan, Ethiopia, na Djibouti. Idadi ya watu wa nchi hiyo ni pamoja na makundi kama Tigrinya, Tigre, Saho, Kunama, Rashaida, Bilen, miongoni mwa wengine, na idadi ya watu wa nchi hiyo ni Wakristo (Coptic, Katoliki, na Kiprotestanti), Waislamu, na dini ya kitamaduni.

Tangu kupata uhuru mwaka 1993, Eritrea imekuwa ikitawaliwa na Rais Isaias Afwerki, ambaye ana mamlaka kamili. Kumekuwa na uhuru mdogo wa kisiasa, na vyama vya upinzani vimepigwa marufuku. Hii imesababisha mvurugo miongoni mwa watu, ambao wanahisi hawana sauti au njia ya kushawishi serikali.

Machafuko nchini Eritrea hasa yanatokana na mchanganyiko wa mambo ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Kwa miaka mingi, nchi imekabiliwa na kutoridhika kwa kiasi kikubwa, hasa kwa sababu serikali inafanya aina ya huduma ya kitaifa isiyodhibitiwa, mara nyingi hujulikana kama "utumwa wa kitaifa." Kwa mfano, vijana wanaandikishwa jeshini, na wengi wanalazimika kufanya kazi katika hali ngumu kwa mshahara kidogo na hakuna mwisho ulio wazi wa utumishi huo.

Uchumi wa Eritrea hauboreki, kwa kadiri kubwa kutokana na mchanganyiko wa vikwazo, ukosefu wa uwekezaji, na sera za serikali ambazo zinazipunguza. Kuna ripoti nyingi za ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na kukamatwa kiholela, mateso, na vikwazo juu ya uhuru wa usemi. Waandishi wa habari, wanaharakati, na wakosoaji wa serikali mara nyingi hufungwa au wananyamazishwa.

Ukandamizaji huo na kufungwa kumewalazimisha watu wengi kutafuta hifadhi au kukimbilia sehemu nyinginezo za Afrika. Watu wengi hao huamua usafiri wa kimagendo kutoka nchini, na mara nyingi hufanya hivyo usiku kwa sababu ya hatari ya kifo au kifungo. Uhamisho huu wa watu wengi umeiacha nchi bila watu walio na ujuzi na umechangia kuzorota kwa kina kikubwa.

Mweritrea mmoja anayehudhuria Mkutano wa Afwid, Dimiana G Habtemariam, 23, ambaye ni mkimbizi USA, alibainisha,

**Mgogoro ulianza:**
Mizizi ya mzozo wa sasa iko katika mvutano wa muda mrefu kati ya Eritrea na Ethiopia, ambao ulianza baada ya Eritrea kupata uhuru kutoka Ethiopia mnamo 1993 kufuatia vita vya miaka 30. Hata hivyo, vita vya mpaka vilianza mwaka wa 1998 na viliendelea hadi mwaka wa 2000, wakati ambapo mkataba wa kusitisha mapigano ulitiwa sahihi lakini hakuna makubaliano ya amani yaliyofikiwa.

**Suala:**
Masuala kadhaa huchochea mgogoro: Migogoro ya mpaka, mvutano wa kikabila na kisiasa na ukiukaji wa haki za binadamu

**Idadi ya Vifo:**
Vita vya Tigray pekee, vinavyohusisha vikosi vya Eritrea, vimesababisha vifo vya watu zaidi ya 600,000 kufikia mwaka 2023.

**Uhamisho:**
Zaidi ya watu milioni 5 wamehamishwa kwa sababu ya mapigano, na milioni 2 wamehamishwa ndani ya Ethiopia na wengi wamekimbilia nchi jirani

*Ndoto yangu kuhusu Eritrea ni kwamba uhuru ambao wale waliokuwa kabla yetu walipigania, utapatikana katika kizazi hiki. Ninaomba Kwamba tutaona Eritrea ikifanikiwa." Aliongeza kuwa "inatia moyo kuwa hapa katika mkutano huu, ili kuona na kujifunza mwenyewe hali za wanawake kote barani. Inashangaza kuona njia zote tofauti za ubunifu ambazo wanawake wanazikazia ili kuleta mabadiliko katika nchi zao.*



## Sudan

Sudan ina makabila mengi, zaidi ya makabila 500. Baadhi ya makundi makubwa ni pamoja na; Waarabu, Wanubi, Beja, Baggara, na wengine wa kabila la Nilo-Sahara wanaoishi kusini, kama vile Nuer na Dinka, na makundi haya hasa wanaishi katika eneo ambayo baadaye ilifanyiza Sudan Kusini.

Sudan ina Waislamu wengi (karibu 97% ya idadi ya watu), na wengi wao wanafuata imani ya Kiislamu ya Sunni. Kuna Wakristo wachache (karibu 3% ya idadi ya watu.) Sudan iko Kaskazini Mashariki mwa Afrika, ikipakana na Misri upande wa kaskazini, na Eritrea na Ethiopia upande wa mashariki. Sudan ina pwani ndefu ya Bahari Nyekundu upande wa mashariki, ikitoa njia muhimu za biashara ya baharini.

Machafuko nchini Sudan yamekuwa yakiendelea na ni magumu sana, hasa tangu Aprili 2023 wakati mapigano yalipoanza kati ya makundi mawili yenye nguvu ya kijeshi, Sudanese Armed Forces (SAF) and the Rapid Support Forces (RSF). Chanzo cha mzozo huu ni kufuatia kupinduliwa kwa Rais wa Sudan Omar al-Bashir Mwaka 2019, ambaye alikuwa ametawala Nchi hiyo kwa karibu miaka 30. Baada ya kung'atuliwa kwake, Sudan iliingia katika kipindi cha mabadiliko makubwa.

> *Tamaa yangu kwa nchi yangu Sudan... ningependa kuona amani ya milele kwa sababu sisi Wasudan, tumeteseka, hasa wanawake na watoto, vurugu. Natamani tu kuwe na amani ya kudumu katika nchi hiyo ili tuweze kuishi kwa furaha na wanawake hawatateseka tena kisiasa, viongozi wa kiraia wanaposhiriki nguvu na jeshi.*
>
> Kaka Jackline Diffala, wa miaka 29.

Vurugu zimeongezeka, hasa katika maeneo ya mijini kama Khartoum, na kuvuruga maisha ya kila siku. Jitihada za kimataifa za kusitisha mapigano zimeshindwa kwa kiasi kikubwa, na hali bado ni tete, zikizua changamoto kubwa katika kutoa msaada kwa watu walioathirika.

**Mgogoro Ulianza:**
Ghasia zilianza Aprili 15, 2023.

**Suala:**
Sababu kuu ya mzozo huo inatokana na mapambano ya mamlaka kati ya majenerali wawili ambao wamekuwa katika muungano dhaifu tangu 2019. Makundi yote mawili yalikuwa yakishindana kudhibiti mpito wa Sudan kufanyiza serikali inayoongozwa na raia

**Idadi ya Vifo:**
Kufikia mwanzoni mwa 2025, idadi ya vifo imezidi 100,000. Kwa kuongezea, mamilioni wamehamishwa ndani na nchi jirani.



## Msumbiji

Msumbiji iko kusini mashariki mwa Afrika, inayopakana na Bahari Hindi upende wa mashariki, Tanzania upande wa kaskazini, Malawi na Zambia kaskazini magharibi, Zimbabwe magharibi, na Afrika Kusini na Eswatini (zamani Swaziland) kusini.

Msumbiji ina makabila mbalimbali, na kuna makabila kadhaa makubwa, kutia ndani Makua, Tsonga, Sena, Ndau, na Shona. Msumbiji hasa ni ya Kikristo na 60-70% ya idadi ya watu hujitambulisha kuwa Wakristo. Pia kuna idadi kubwa ya Waislamu, hasa katika maeneo ya pwani, ambayo ni karibu 20% ya idadi ya watu. Dini za kitamaduni za Kiafrika zinafanywa na asilimia ndogo ya idadi ya watu. Machafuko nchini Msumbiji, haswa katika mkoa wa kaskazini wa Cabo Delgado, yamekuwa makubwa sana na yalianza karibu 2017 na yanaendelea kusababisha uharibifu mkubwa.

Tofauti za kiuchumi na malalamiko ya ndani — licha ya Msumbiji kuwa tajiri katika rasilimali za asili—hasa hifadhi za gesi asilia za pwani—kwa muda mrefu zimevuruga Cabo Delgado, moja ya mikoa maskini zaidi Nchini Msumbiji. Mzozo ulipoongezeka, makundi ya wanamgambo, ikiwa ni pamoja na makundi ya ISIS, yalianza kutia mizizi katika eneo hilo.

Serikali ya Msumbiji imejitahidi kudhibiti uasi huo, ikitegemea sana mikakati ya kijeshi. Vikosi vya usalama vimekosolewa kwa kufanya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mauaji kiholela uhamishaji wa kulazimishwa. Mwaka 2021, serikali ilialika misaada ya kigeni, hasa kutoka kwa vikosi vya Rwanda na SADC (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika), ambayo vilisaidia kuchukua tena miji muhimu na kurejesha hali ya utulivu.

Hali bado ni hafifu sana, na ingawa kuna juhudi za kuleta amani, hakuna dalili ya utatuzi madamu masuala nyeti—ukosefu wa usawa wa kiuchumi, ukosefu wa haki, na misimamo mikali-kubaki haziangaziwi. Mzozo huo umeharibu jamii za mitaa, na kuwaacha mamilioni bila mahitaji ya msingi, na kuathiri sana maisha ya watu wa Msumbiji. Kwa mfano, mjumbe Celina Benjaminim Dos Santos Mataca, 49, anasema:

> *Kila kitu ni ghali sana: chakula, nishati, maji... katika azma yangu kwa nchi yangu, natamani bei za vitu zipungue ili kila mtu aweze kuzinunua. Leo, huwezi kununua vitu kama kuku, kwani ni ghali sana*

**Mgogoro Ulianza:**
Ghasia zilianza Oktoba 2017.

**Suala:**
Mzozo huo unachochewa na mchanganyiko wa mambo, kutia ndani ukosefu wa usawa wa kiuchumi na kijamii.

**Idadi ya Vifo:**
Kufikia mwaka 2025, makadirio yanaonyesha kuwa zaidi ya watu 4,000 wameuawa, na karibu milioni 1 wamehamishwa kwa sababu ya vurugu.

## DRC

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ina makabila zaidi ya 200. Vikundi vikubwa zaidi vinatia ndani Luba, Mongo, Kongo, na Watutsi, miongoni mwa vikundi vingine vingi.

Kwa miaka mingi, mzozo nchini DRC umeenezwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mauaji ya halaiki, unyanyasaji wa kijinsia, na kuhamishwa kwa nguvu. UM imedumisha kikosi kimoja cha jeshi lake kubwa (MONUSCO) ili kulinda amani nchini DRC tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000, lakini licha ya uwepo wao, vurugu zimeendelea.

DRC imepambana na utawala dhaifu, ufisadi, na taasisi zisizofaa. DRC hasa inatambulika kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali, madini kama coltan, almasi, na dhahabu. Hata hivyo, rasilimali hizi zimevutia uingiliwaji wa ndani na wa nje, hivyo kuchochea migogoro ya rasilimali.

Mzozo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) una mambo mengi na umekita mizizi katika mchanganyiko wa mambo ya kihistoria, kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Hapa kuna sababu za msingi za mzozo unaoendelea; pamoja na urithi wake wa kikoloni, mvutano wa kikabila na siasa za kitambulisho, uingiliaji wa kigeni, vikundi vya waasi na wanamgambo wenye silaha, kutaja chache tu. Kwa muhtasari mzozo nchini DRC unaweza kufafanuliwa kuwa matokeo ya mchanganyiko wa changamoto za kihistoria, mapambano ya udhibiti wa rasilimali, mvutano wa kikabila, utawala dhaifu, na uingiliwaji wa kigeni.

Uundaji wa idadi ya WATU WA DRC, pamoja na mambo ya kihistoria, kisiasa, na kiuchumi, umeunda mazingira tete ambapo watendaji mbalimbali, wa ndani na nje, wamechangia mzozo unaoendelea. Kutatua masuala haya kunahitaji kuangazia udhaifu wa utawala, kukuza mazungumzo ya kitaifa, na kusimamia ushindani juu ya rasilimali kwa njia ambayo inawanufaisha watu wote wa Kongo, sio watu mashuhuri pekee au wanaotoka nje. Bambe Cikunda Annie alielezea hamu yake kwamba "Kwa ufupi, ningependa kuona nchi yangu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ikiwa nchi ambako amani inatawala. Ambako wanawake na wasichana wanaishi kwa heshima, na unyanyasaji dhidi ya wanawake na ubakaji haupo tena katika nchi yangu, DRC."

**Mgogoro Ulianza:**
Mzozo wa sasa ulianza wakati wa Vita vya Pili vya Kongo (1998-2003), ambayo ilihusisha nchi nyingi jirani. Uasi wa sasa ulianza Aprili 2012

**Suala:**
Mzozo mashariki mwa DRC unachochewa na mchanganyiko wa mambo, ikiwa ni pamoja na mvutano wa kikabila, udhibiti wa rasilimali, serikali kuu dhaifu na maslahi ya kikanda

**Idadi ya Vifo:**
Ni vigumu kukadilia idadi ya vifo katika mzozo wa mashariki mwa DRC haswa kwa sababu ya hali ya vurugu ya muda mrefu. Walakini, inaaminika kuwa tangu kuanza kwa mzozo mwishoni mwa miaka ya 1990, zaidi ya watu milioni 5 wameuawa.



# WAJUMBE KUTOKA ZAMBIA KULETA TAHADHARI KWA MAHITAJI MAALUM

NA NONKULULEKO MURAVHA





Wajumbe kutoka Zambia walivurugika kidogo wakati wa mchakato wao kabla ya kutua Afrika Kusini kwa Mkutano wa 3 wa kila mwaka wa AFWID.

Tulipowakaribisha wajumbe wa Afwidi Afrika Kusini, tukiwapokea katika uwanja wetu wa ndege wa kimataifa OR Tambo, na kukutana nao kwa mara ya kwanza kabisa, tuliweza kutambuana kwa chapa yetu nzuri na tabasamu zao zenye kuvutia.

Katika hali ya sherehe na zaidi ya msisimko wa kutua Nyumbani, wanawake wa Zambia walielezea mvurugo waliopata kuhusiana na upatikanaji wa malazi kwa wajumbe wao walemavu.

Kulingana na mmoja wa wajumbe wa Zambia, Muka Nyambe, 33, ambaye pia ni mratibu wa ujumbe wa Zambia, walipokuwa karibu kupanda ndege, hawakufikiria kuwa kutakuwa na changamoto yoyote kwa wanaotumia viti vya magurudumu, lakini mara tu walipokuwa kwenye ndege, hawakuweza kupata huduma za viti vya magurudumu na hiyo karibu hilo lingechelewesha ndege, lakini kwa bahati nzuri wafanyikazi wa Shirika la Ndege la Afrika Kusini walisaidia mara moja, waliomba msamaha, na wakaandaa mahitaji ya abiria hao.

Muka alishiriki maneno machache kwa watu ambao wanapanda ndege kwa mara ya kwanza kabisa. Moja ya vidokezo alivyoshiriki ni kwamba unapaswa kubeba vitu muhimu kila wakati kama dawa ya maumivu ya kichwa na homa na kwamba abiria wanapaswa kusikiliza kwa uangalifu maagizo yote yaliyotolewa na wafanyikazi na kuzingatia vidokezo vyote.

Aliongeza, "hakukuwa na masuala ya hali ya hewa yaliyoripotiwa, na hali zilikuwa nzuri" ambayo ilisababisha kutua salama na hata dakika 20 kabla ya muda uliokadiriwa, kuruhusu wajumbe kukutana na kusalimiana na kufurahia mkutano pamoja.

# UJUMBE WA SAWID KUUNGA MKONO AFWID



**Ujumbe wa Kuunga Mkono AFWID wa 2025**

Bodi ya Wadhamini ya Mjadala wa Wanawake wa Afrika Kusini (SAWID) inakuandikia kwa heshima kubwa kama shirika dada na lako linalojivunia kuwa katika ngazi ya kitaifa. Tunakupongeza wewe na timu yako kwa dhati kwa kufanikiwa kukusanya wanawake 1,000 kutoka nchi 55 za Afrika kwa mara ya pili katika miaka sita.

Katika msimu huu ulioathirika kisiasa dhidi ya wanawake, wenye upungufu unaoendelea kila siku wa kanuni za haki na mshikamano, na athari inayoonekana dhidi ya usawa wa kijinsia na ajenda ya wanawake, ikikusudiwa kunyamazisha sauti za wanawake, tumehamasishwa sana na wonyesho huu wa uanaharakati wa kijinsia na wanawake wa Kiafrika, wanaofanya juhudi za kushikana mikono na kufanya kazi pamoja.

Ni rahisi sana kukatishwa tamaa kufuatia kushuka kwa amani duniani na kuongezeka kwa unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya wanawake, lakini unatuongoza kutambua ongezeko la idadi ya viongozi wa wanawake katika maeneo mbalimbali ya bara la Afrika na duniani.

Maendeleo ya Malengo ya Maendeleo Endelevu: Ripoti kuhusu Jinsia 2024 ya Umoja wa Mataifa ilionyesha kuwa wanawake sasa wanashikilia moja katika kila viti vinne vya bunge ulimwenguni, na idadi ya wanawake na wasichana wanaoishi katika umaskini uliokithiri imeshuka chini ya 10%.

Hata hivyo, kwa kusikitisha, hakuna hata moja ya viashiria vya Lengo la 5 la SDG, lengo la Usawa wa Kijinsia, limetimizwa. Takriban msichana mmoja kati ya 4 wanaendelea kuozwa wakiwa watoto, na itachukua takriban miaka 137 kuwatoa wanawake na wasichana wote kutoka kwenye umaskini.

Mafanikio yako makubwa hayasisitizi tu nguvu na umoja wa wanawake kote bara bali pia yanaonyesha nguvu ya ushirikiano na maono yako ya kuwekeza katika sauti za wanawake wa Kiafrika ili kushughulikia changamoto nyingi nyeti ambazo bado zinakabili nchi yetu, bara letu na ulimwengu leo, pamoja na viwango vilivyo wazi vya ukosefu wa usawa na umaskini, na kuongezeka kwa changamoto za kijamii na kiuchumi ambazo kila siku huathiri maisha ya wanawake wa Kiafrika na familia zao.

Mpango wako wa kuleta pamoja sauti za wanawake kutoka Afrika nzima ni utambuzi mkubwa wa jukumu muhimu ambalo wanawake hutimiza katika kuleta mabadiliko, sio ndani ya jamii zao tu, bali katika ulimwengu mzima. Kwa sisi kama Wanasawidi, mjadala huu ni sherehe ya hatua za kubwa ambazo wanawake wamechukua, na ni wito wa kuendelea kuchukua hatua, kwa sababu safari inaendele ya kupata ulimwengu wa haki, usawa, amani, na upendo.

Tunathamini sana jukumu la WDB Trust na AFWID kuhakikisha amani ndiyo msingi wa maendeleo ya wanawake. Msingi wa amani huanza kitengo cha familia, ambapo wanawake mara nyingi hutumika kama walezi wa msingi na wajumbe wa amani. Kwa kukuza mazingira yenye maelewano, umoja, na uthabiti katika kiwango cha familia, tunaweza kujenga jamii yenye nguvu na usawa zaidi kwa vizazi vijavyo.

Kwa kuongezea, tunapongeza kujitolea kwako kupata suluhisho zinazoonekana ambazo zitaongeza ustawi wa jumla wa wanawake wa Kiafrika na familia zao, zinazoshughulikia mahitaji yao kamili ya ukuaji, usawa, na ubora wa maisha.

Katika SAWID, tumejitolea kusimama nawe katika juhudi hizi njema. Tunaahidi kwamba hatutayumba-yumba katika kuchangia mafanikio ya mpango huu. Tungependa kuhusika kikamilifu katika mazungumzo kabla, wakati, na baada ya tukio hili, kupaaza sauti yetu, rasilimali, na mshikamano ili kuendeleza malengo ya pamoja tunayoyapenda.

Kazi yako inatutia moyo sisi sote, ikitukumbusha uwezo wa mabadiliko ya wanawake waliounganishwa kwa kusudi na hatua ileile. Tafadhali tutegemee kama washirika thabiti katika dhamira yako ya kuinua, kuwezesha, na kuleta mabadiliko ya kudumu kwa wanawake na familia zao kote barani na kwingineko.

Kwa heshima na kwa mshikamano.

**Bi. N.F. (Thoko) Mpumlwana**
Mwenyekiti wa Bodi ya SAWID

**Bi. Vatiswa Moea**
Mkurugenzi Mtendaji SAWID

# WANAWAKE WA AFRIKA WAUNGANA KATIKA MKUTANO WA TATU WA MJADALA WA WANAWAKE WA AFRIKA

## NA NKHENSANI NKHWASHU





Mkutano wa Tatu wa Mjadala wa Wanawake wa Afrika (AFWID) ulianza Jumatatu na kuleta pamoja sauti zenye ushawishi na watunga mabadiliko kutoka bara zima.

Tukio hilo lilianza kwa maneno ya kukaribisha kutoka Riah Phiyega, Mkurugenzi Mtendaji Wa WDB Trust. Phiyega alionyesha kwamba mandhari "Sauti ya wanawake na nguvu yao kama mawakala wa mabadiliko" inasisitiza uharaka wa hatua ya pamoja kama kipaumbele kwa wanawake wote. "Tunapokusanyika hapa, tunakumbushwa juu ya hatua ambazo tumefanya na changamoto ambazo bado ziko mbele. Jitihada zetu za pamoja ndizo zimetufikisha hapa, lakini bado kuna mengi zaidi ya kufanywa. Lazima tuendelee kama wanawake kushinikiza sera zinazotuwezesha kiuchumi, kijamii, kisiasa na vinginevyo. Lazima tupinge vizuizi vya kimfumo ambavyo vinazuia maendeleo yetu na lazima tuungane katika mapambano yetu dhidi ya kutengwa na unyanyasaji wa kijinsia."

Phiyega alizungumzia changamoto zinazowakabili wanawake katika vijiji vya mashambani kote barani. "Wanawake hawa ni uti wa mgongo wa jamii zao lakini watu hawatajua, wanafanya kazi bila kuchoka na mara nyingi bila kupewa elimu ya kutosha, bila huduma za afya na fursa za kiuchumi. Wanaathiriwa sana na umaskini, ukosefu wa miundombinu na athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Mara nyingi sauti zao hazisikiki na mahitaji yao hayatimizwi."

Alizungumza kuhusu umuhimu wa kuunda nafasi salama kwa wanawake kujimudu na kuwa na uwezo wa kuwa mawakala wa mabadiliko. Pia aliwahimiza wanawake kuhamasishana ili kuwa vichocheo vya mabadiliko.

Katika ujumbe wake wa kuunga mkono, Dk Nkosazana Dlamini-Zuma, mwenyekiti wa zamani wa Umoja wa Afrika, aliangazia changamoto zinazowakabili wanawake wengi barani humu ambazo huzuia sauti zao kusikika. Alisema wanawake wengi hawana sauti kwa sababu ya umaskini, akisisitiza haja ya kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini.

Zaidi ya hayo, alisisitiza kwamba kupata elimu na kupata ujuzi husika huwa ni changamoto kubwa. Alibainisha kuwa ni muhimu kwamba ujuzi huu utumiwe kujenga fursa za kiuchumi, kwa vile wanawake katika nchi nyingi hukabiliwa na kikwazo kikubwa ambacho ni upatikanaji mdogo wa rasilimali za kifedha.

Pia aliunga mkono msimamo wa Phiyega kwamba ukosefu wa huduma za afya ni changamoto kubwa.

Mwenyekiti wa Mjadala wa Wanawake wa Afrika Kusini (SAWID) ambayo ni shirika dada na AFWID, Thoko Mpumlwana alisema: "Mkutano huu hufanyika wakati ambapo siasa za kijiografia ni changamoto kwa wanawake katika bara letu, haswa katika Mashariki ya Kati. Tunachoogopa, ni mmomonyoko wa haki, mshikamano na pigo la usawa wa kijinsia na ajenda ya kike. Kwa hivyo tunapokusanyika hapa, tunajikumbusha kwamba lazima tushikane mikono na kuwa katika kushikamana kila wakati. Malengo ya maendeleo endelevu yametuambia kwamba kati ya mambo mengine mengi, lazima tuhakikishe umaskini unapigwa vita "

Pia aliwahimiza wajumbe waendelee kupigania usawa wa kijinsia kabla ya kuahidi mshikamano na msaada wa SAWID kwa AFWID. "Tutakuwa hapa wakati wote, tukipaaza sauti yetu, rasilimali, mshikamano na ninyi. Kazi yenu inatutia moyo na tunawatakia mema, Afrika ni nyumbani - acheni tuifanye itende."



Akihutubia wajumbe hao, Dkt. Stellah Bosire, mwanaharakati wa haki za binadamu, daktari na mwandishi Kutoka Kenya aliwashukuru maveterani waliofungulia wanawake vijana njia. "Bila nyinyi singekuwepo nasi tupo kwa sababu ninyi mpo. Wanawake hawa wametupatia sauti, uwepo, na uhakika."

Alisema urithi wao umewahimiza wanawake kukusanyika chumbani kwa ujasiri kufafanua upya mazingira ya uongozi wa wanawake na kukuza sauti ambazo zimenyamazishwa kwa muda mrefu sana. "Asanteni sana kwa kutayarisha njia."

Pia aliwashukuru wanawake ambao juhudi zao bila kuchoka zinaendelea kuchochea dhamira ya kuendelea kuchapa kazi. "Nguvu zenu, maono yenu na ujasiri wenu hututia moyo sisi sote."

Dkt. Bosire pia alizungumza juu ya shambulio dhidi ya mashirika ya wanawake na watu wa jinsia tofauti akisema ni suala lililo sehemu ya majidiliano nyeti linalohangaisha ulimwengu.

"Wanawake katika utofauti wao wote wanakabiliwa na kuongezeka kwa vurugu na ukandamizaji, unaosababishwa na mamlaka zenye nguvu ndani ya harakati za kupinga jinsia. Harakati hii, inayochochewa na uongozi wa kifashisti na wa kimabavu, inaongozwa na muungano wa vikundi vitatu vya kihafidhina: serikali, taasisi za kidini, na mashirika ya kiraia. Kwa ushirikiano wamebuni mfumo wa pamoja unaolenga kufinyilia haki za wanawake na watu wanaopigania mpanuko wa jinsia."

# ROHO YA UMOJA ILIONEKANA KATIKA MAVAZI YENYE RANGI NYINGI

## NA LINDOKUHLE MAINDY MABENA

Mandhari ya siku hiyo ilionyesha urembo wa Kiafrika, roho ya umoja, na ubuntu wajumbe kutoka nchi 55 wa Afrika walipofika kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa OR Tambo.

Jumapili, Januari 26, 2025, wanawake walifika katika vikundi vya watu 16 mapema asubuhi, mapema saa 03:55 asubuhi, wakiwa wamevalia mavazi ya rangi maridadi sana. Wajumbe wa nchi nyingi walionekana kwa rangi moja, wakiashiria umoja kati ya wajumbe ambao wote waliwasili katika roho ileile, wakiwa wamejaa msisimko.

Maimuna Secka, 48, kutoka Gambia alisema kwamba hii ilikuwa mara yake ya kwanza kuwa katika mkutano wa Mjadala wa Wanawake wa Kiafrika, lakini alihisi ukaribishaji mchangamfu wa dada wote kutoka nchi zingine kwani wote walitua kwenye uwanja wa ndege uleule na wajumbe wote wakawa kitu kimoja, bila kujali ni nani aliyefika kutoka wapi.

Sinah Masemola, Mratibu wa Mjadala wa Wanawake wa Afrika Kusini kutoka Limpopo, 55, alisema kwamba kuwa Mwafrika humaanisha umoja, na kwa hivyo, "ikiwa wanawake hawajaunganishwa, hakuna kinachotatuliwa," aliongeza kuwa hii ni fursa adimu sana ambapo wanawake hujivunia, hufurahia uhuru na ubora wa Kiafrika.

Dumi Gatsha, 34, mwanzilishi wa kampuni inayoitwa Success Capital huko Botswana, alisema walifurahi kwamba kuna wanaharakati wengine wengi wa kike ambao wamekutana katika miaka mitano iliyopita na walithamini kutojitambulisha kwa jinsia fulani hususa, amabo wamehudhuria AFWID, "Nadhani ni muhimu sana, kutafakari tu miaka mitano baadaye, kwamba tutakuwa hapa na kuungana watetezi wa haki za Afrika."











# WANAWAKE WENYE USHAWISHI AFRIKA WAFUNGUA NJIA YA SIKU ZIJAZO KATIKA KIAMSHA KINYWA CHA AFWID 2025

NA AKHONA VALASHIYA

Mkutano wa Mjadala wa Wanawake wa Kiafrika (AfWID) wenye ushawishi ukiendelea, siku ya pili ya mkutano huo ilianza na kiamsha kinywa kati ya wajumbe wa AfWID na WDB Board of Trustees, na viongozi wanawake kutoka nchi 55 za Kiafrika zilizowakilishwa.

Chini ya utambulisho'Sauti za wanawake wakiwa mawakala wa mabadiliko,' mazungumzo yalianza kwa maelezo ya ya washiriki wakikumbuka mkutano wa Jukwaa la Beijing la Utekelezaji kisha yakaongezeka ili kuimarisha Harakati za Wanawake wa Kiafrika, na yalichanganua mwendelezo wa uendelevu wa AfWID kama jukwaa la kuchangia utatuzi wa migogoro na kudumisha amani Barani Afrika.

(Kwa ufupi, Azimio la Beijing la 1995 na Jukwaa la Utekelezaji lake lilipitishwa na nchi 189 ulimwenguni kama gurudumu la kuendesha uwezeshaji wa wanawake na wasichana.)

Miongoni mwa wengi wa waliokuwepo kwenye kiamsha kinywa ni mwanasiasa na mtaalam Mnaigeria, Dkt. Agary Timiebi Augusta Koripamo, ambaye aliongoza Mpango wa Utekelezaji huko Beijing mnamo 1995. Dkt. Timiebi ni mhusika mkuu wa mijadala ya wanawake. Hii ilikuwa dhahiri katika maneno yake aliposema, "Lazima tuendelee kama wanawake kushinikiza mazungumzo na lazima kusiwe na mbadala wa mazungumzo."

Kuwakaribisha wajumbe, MamaMbeki aliwasihi wote waliokuwepo katika kifungua kinywa kuhamasisha matumizi ya juhudi sawa katika jaribio la kutatua mzozo Nchini Msumbiji – kama ilivyofanyika katika Majadiliano ya Amani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Siku AfWID ilipoanzishwa, Mama'Mbeki, anasema lilikuwa wazo lilitokana na mkutano wa kwanza wa wanawake katika nchi wanachama wa Southern African Development Countries (SADC). "Ilikuja akilini kwamba ni lazima tuwaunganishe wanawake wa SADC ili tufanyize ajenda yetu wenyewe badala ya ile iliyofantizwa na wengine", alisema Mama'Mbeki.

Kiamsha kinywa hiki kilitumika kama nguvu ya kuchochea roho za shauku za mashujaa wanawake-viongozi wanawake katika bara lote la Afrika.









# MAJADILIANO YA JOPO KUHUSU WAKATI UJAO TUNAOTAKA: MASWALI NA MAJIBU NA MAPENDEKEZO

NA HAWA MAYERE

**Swali**
"Michal, kama mtu anayetoka nchi unayopenda sana, lakini huwezi tena kurudi kutokana na migogoro, ungewaambia nini wakimbizi wengine-wale ambao wamelazimika kukimbia au kubaki mbali na nchi zao kwa sababu ya kutokuwa na utulivu wa serikali na usumbufu? Tunawezaje kuendelea kupigania na kuunga mkono nchi zetu tukiwa mbali?"—Marie Justine Mpano Mutabazi, 21, Rwanda

**Jibu-Michal Petros**
"Kusimulia hadithi ni zaidi ya njia ya kuhifadhi utamaduni; ni chombo chenye nguvu cha kuishi na kujieleza, hasa katika mazingira kandamizi. Vyombo vya habari vya ughaibuni vina jukumu muhimu katika kutoa sauti kwa wale walionyamazishwa nyumbani. Shirikiana na mashirika yanayoandaa nafasi ambapo unaweza kukosoa na kujadili maendeleo.

Kugeuza maumivu na mapambano kuwa hadithi yako ya kibinafsi ni kitendo kikubwa cha kukaidi. Kwa kushiriki hadithi yako, zaidi ya kuhifadhi utamaduni wako, unapigania nchi yako pia, hata ukiwa mbali.

**Swali:**
"Tunawezaje kupaaza zaidi sauti za wanawake wenye ulemavu katika mijadala, na ni hatua gani tunaweza kuchukua kuhakikisha ujumuishaji wa kweli na usawa kwa wanawake wote walemavu?"- Maseray Brima, 41, mjumbe kipofu kutoka Sierra Leone

**Jibu: Jennifer Abomnger**
Ingawa walemavu mara nyingi huwakilishwa katika majadiliano, si kila wakati wamejumuishwa kikamilifu au wanashirikishwa ifaavyo. Lengo huwa ni kuonyesha uwezo badala ya kuandaa mahitaji muhimu mbalimbali kwa walemavu. Katika mazingira mengi, ikiwa ni pamoja na Afrika, uelewaji wa ulemavu ni haba, na watu wengi hufikiri kuhusu ulemavu wa kimwili tu. Hilo linapuuza aina nyingine nyeti za ulemavu, kama vile ulemavu wa akili, kiakili, na kisaikolojia. Ili kuhakikisha ujumuishaji sahihi na usawa, ni muhimu kutambua na kushughulikia mahitaji ya kipekee ya wanawake wote wenye ulemavu, kutetea nafasi zinazopatikana, kuandaa msaada mahsusi, na ujumuishaji wa sauti zote kwenye majukwaa yote.






**Mapendekezo ya hatua za kuchukua**
***Mapendekezo ya Wakili Thando Gumede:***
Alikazia umuhimu wa kurejesha heshima na thamani ya wanawake, ambao kihistoria wamekuwa sehemu nyeti katika maisha ya kiuchumi ya familia za Kiafrika.

Aliongeza zaidi haja ya kuimarisha familia na jamii za Kiafrika, akisisitiza umuhimu wa kila mtu kuelewa jukumu na jukumu lake katika jamii. Hii ni pamoja na kufanya kazi pamoja kwa umoja, kuandaa maendeleo, na kukubali kwamba sio kila mtu atakuwa kiongozi, lakini kila jukumu ni muhimu.

Alisisitiza jinsi wanawake vijana wa Kiafrika walivyohitaji kuchukua uongozi, wapange siku zijazo, watumie teknolojia na rasilimali kwa uwajibikaji ili kuendesha mabadiliko.

Yvonne Muma Bih kutoka Cameron alitetea Afrika huru, ambapo watoto Waafrika wanaweza kusafiri kwa uhuru, kufanya biashara, na kupata elimu katika bara lote. Anaamini kuwa Afrika iliyoungana na yenye nguvu zaidi, na uongozi na sauti za wanawake, zitashinda vizuizi vya ukoloni mpya na kuongoza ulimwengu katika mustakabali bora.

# KUJIHUSIANISHA KIBINAFSI NA WENGINE

NA LINDOKUHLE MABENA



Jumatatu, Januari 27, 2025, ilikuwa siku ya kwanza ya mkutano wa Tatu wa kikao cha  Mjadala wa Afrika, wakati ambapo washiriki waligawanywa katika vikundi ili kuhudhuria vikao vilivyokusudiwa kuwaunganisha na wengine.

Katika vikao hivi, washiriki walitafakari kwa undani juu ya maono yao na uhusiano wao na wengine kupitia mazoezi ambayo yanachochea mawazo na uzoefu wao wa masuluhisho.

Wakati wa vikao, uvumba ulichomwa, na mishumaa iliwashwa, kila moja ikiashiria maana tofauti kulingana na rangi yake, ikitegemea wawezeshaji...

- Mshumaa wa kijani unaashiria ustawi, mafanikio, na afya.
- Mshumaa wa manjano unaashiria werevu, umakini, ujifunzaji, vizuizi vya akili, hekima, uwazi, ujasiri, na mantiki.
- Mshumaa wa rangi ya waridi unaashiria upendo usio na masharti, joto, kujipenda, upatanisho, urafiki, na furaha.
- Mshumaa wa bluu unaashiria uponyaji wa kihemko, mawasiliano, ubunifu, umakini, haki, msukumo, maelewano, na amani ya akili.
- Mshumaa mweupe unaashiria utulivu, uponyaji, kufanywa upya, na utakaso.

Mkazo ulikuwa juu ya maisha kama safari, ikiwa ni pamoja na historia ya mtu, na labda uzoefu wowote wa kiwewe ambao mtu angependa kupona. Washiriki walipewa kazi ya kufuatilia njia ya maisha waliochagua kisha wapake rangi kulingana na jinsi walivyopendelea. Mgawo huu ulikusudiwa washiriki kutafakari kuhusu safari yao ya maisha, walikotokai, ni wapi hawajawahi kuwa, na wapi wangependa kuwa. Mratibu wa Mazungumzo wa Wanawake wa Afrika Kusini katika jimbo la Fee-State (Afrika Kusini), Francinah Sehlabaka, alishiriki kwamba ni muhimu kuwa na miundo ambapo wanawake hufurahia kusuruhisha majeraha yao ya moyoni, kushiriki upendo, na kuwawezesha kila mmoja. Sehlabaka alisema jinsi tunavyohisi huamua kile tunaweza au hatuwezi kufanya nyakati zote, kwa hivyo ni muhimu kwa watu binafsi kuwa na vipindi vya kibinafsi vya kutafakari na kuungana tena na wengine.

Kipindi cha tatu kilihusisha kuandika mambo ambayo washiriki walitaka kuachana nayo na kufungua nafsi zao ili kupokea upendo usio na masharti kutoka kwa wanawake wenzao. Kila mmoja alipewa karatasi safi ya kuandika yote ambayo anapaswa kuachana nayo, akakunja karatasi hiyo, na kuirarua vipande-vipande. Kupasua kuliashiria kuacha msururu wa tabia mbaya au mambo mengine ambayo yanaweza kuwa kizuizi katika maisha yao. Anago Judicial Grace, 40, Kutoka Benin, alisema kuhudhuria kikao cha kujitenga ni jambo ambalo alipaswa kufanya muda mrefu uliopita kwa sababu kuzungumza kwa njia hii hufungua njia inayoelekeza kwenye mwanga katika maisha.

# KUVAA HADITHI ZETU KWA MTINDO

Tulipokusanyika pamoja katika maeneo ya Birchwood, nyumba yetu kwa siku tano tukufu za mwingiliano wa wanawake wenye nguvu, tafakari na hekima, tulifanyiza mahali hapa kuwa kwa mavazi yetu. Karibu kila kona, WaAfWIDi walionyesha mifumo ya rangi mbalimbali kupitia nguo nzito na zinazotiririka na changa zinazomelemeta. Tulibeba mtindo wetu wa kibinafsi kwa urahisi, tukizingatia umaridadi kwenye mkusanyiko huu na kuonyesha kuwa mitindo kupitia lebo, na pia kupitia mavazi yanayoashiria hadithi zetu.





















# USTAWI WA KIUCHUMI KATIKA ULIMWENGU WA KIBEPARI: JE, WANAWAKE WAAFRIKA WANAWEZA KUSTAWI KWELI?

NA HAWA MAYERE

Katika 2025 swali la iwapo wanawake wa Kiafrika wanaweza kustawi na kushiriki katika “mfumo wa uchumi unaostawi” halihitaji majibu.

Hata hivyo, kutokana na historia kwamba kwa kweli mfumo wa kiuchumi uliundwa kwa njia ambazo mara nyingi zilipunguza upatikanaji wa rasilimali na fursa kwa Waafrika, inaonyesha kwamba makundi ya wanawake wa Kiafrika waliotelekezwa wanakabiliwa na hasara nyingi mno.

Ili wanawake wa Kiafrika wastawi, kuna uhitaji wa kukabiliana na vizuizi vya kimfumo, kuunda mshikamano, na kupata njia za uwezeshaji na msaada ili kufikia maendeleo endelevu na uvumbuzi.

Wakati wa kikao, maswali mawili muhimu yaliulizwa ambayo yaliangaza kuhusu njia bora ya kusonga mbele kama wanawake wa Kiafrika katika ulimwengu wa kibepari.

**Ustawi wa kiuchumi unamaanisha nini katika maisha yako ya kibinafsi?**

Inahusisha kupunguza kabisa umaskini, kuunda utajiri wa kizazi, na kuchangia mabadiliko ya kitamaduni kwa njia pana ambapo wanawake watachukua majukumu nyeti. Ustawi wa kweli wa kiuchumi unamaanisha kuishi kwa kusudi, na ufikiaji wa rasilimali zote muhimu ili kufikia maono.

Akiongeza maoni kutoka kwa waliohudhuria, Wakili Brenda Madumise, 60, kutoka Afrika Kusini alisema, “Mfumo wa sasa ulibuniwa ili kuvuruga usawa.” Alikazia jinsi miundo ya sasa ya kiuchumi imeundwa ili kunyakua, na kwamba wanawake weusi hasa, wamenaswa katika dimbwi la umaskini na unyanyasaji.

Akirudia hisia za mjumbe mmoja, Lando Dlamini (35) kutoka Eswatini alibaini kuwa “ustawi wa kiuchumi hauhusu tu uundaji wa utajiri, lakini pia unahusu kuthamini michango anuwai na kuondoa mifumo ambayo kihistoria imetenga au imedharirisha vikundi fulani”

**Mshikamano wa kiuchumi unamaanisha nini na unadhihirikaje katika maisha halisi?**

Mshikamano wa kiuchumi mara nyingi hurejelea uungwaji mkoni wa pamoja kwa wanawake na jamii ili kuimarisha nguvu za kiuchumi pamoja. Katika Afrika Kusini neno Stokvel linahusu klabu ya akiba ya jamii ambayo husaidia katika kuimarisha mshikamano wa kiuchumi ndani ya jamii.

Jambo lingine muhimu ambalo lilijadiliwa ili kuimarisha zaidi ustawi wa kiuchumi katika jamii ya kibepari lilikuwa:

- Majukwaa ya dijititali ya mshikamano wa kiuchumi ambayo yanapaswa kusaidia kufadhili watu kwa biashara zinazoongozwa na wanawake na kuhamasisha zaidi kwa mitandao ya kugawana rasilimali kwa ushiriki mkubwa wa wanawake wa Kiafrika katika mfumo wa uchumi, ili kustawi.
- Ujuzi na nafasi za kubadilishana maarifa ambapo watu wanaweza kubadilishana huduma au maarifa ili kukuza uchumi kwa kusaidiana.

Kwa kumalizia, ilipendekezwa kuwa kwa ushirikiano wa wanawake wa bara, ni muhimu kuunda vikundi vya akiba, ambavyo vinaweza kuanzisha mpango wa kisasa wa kuandaa mikopo kwa jamii, ambapo vikundi vidogo vya watu vitachanga bila kutozwa riba, wakizingatia vikundi vilivyotengwa au vilivyo hatarini kiuchumi.



# KUFIKIRIA UPYA 'MUSTAKABALI WETU ZAIDI YA BEIJING'

## NA LINDOKUHLE MABENA

Mkurugenzi wa programu Mildred Ngesa, mwandishi wa habari aliyeshinda tuzo, mtaalam wa vyombo vya habari na mawasiliano na mkufunzi wa uongozi wa mabadiliko, alikuwa msimamizi wa majadiliano ya jopo siku ya pili ya mkutano, na alifungua kikao kwa nukuu, "Vijana wanaweza kutembea haraka, lakini wazee wanajua njia." Kisha akatambulisha washiriki wa jopo, pamoja na wanawake walishiriki katika Azimio la Beijing la 1995 na Platform for Action (PFA).

Mwaka wa 2025 unahitimisha miaka 30 baada ya Mkutano wa Beijing, ambao ulianzisha malengo na vitendo vya kimkakati kwa maendeleo ya wanawake na mafanikio ya usawa wa kijinsia katika maeneo 12 muhimu ya hangaiko kama vile wanawake na umaskini, elimu na mafunzo kwa wanawake, wanawake na afya, unyanyasaji dhidi ya wanawake, wanawake na migogoro ya silaha, wanawake na uchumi, na wanawake katika mamlaka na maamuzi.

Jopo hilo lilikagua maendeleo yaliyofanywa tangu azimiio hilo na likachunguza njia mpya za kuendeleza usawa wa kijinsia kote Afrika.

Washiriki wa jopo walikuwa Dan Entseya Mtaalami w kiuchumi, Mchambuzi Wa Sera za Umma Kutoka Senegal, Jennifer Abomnger Mtetezi wa Ujumuishaji wa Walemavu, mwezeshaji wa Afya ya Ngono na Uzazi, Na mtetezi wa haki ya hali ya Hewa kutoka Nigeria, Michal Petros, Mpiga Picha, Meneja wa Mradi anayehusika katika Ujenzi wa Jamii kutoka Eritrea, na Mtetezi Thando Gumede Kamishna wa Afrika Kusini wa Usawa wa Jinsia na Nagwa Ibrahim, Mwanzilishi na Afisa Mkuu Mtendaji wa Edraak Foundation for Development and Equality, kutoka Misri. Pia anaongoza Kikundi cha Vijana Wanawake.










# WANAUME KAMA WASHIRIKA WA AFWID

## NA LEBOGANG MATHEBULA



Katika bara lililojaa ukatili dhidi ya wanawake, umaskini na ukosefu wa usawa wa kijinsia, kupokea msaada kwa wanawake ni hatua muhimu ya kukomesha maswala haya yote. Wanawake Barani Afrika wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, sio tu duniani kwa ujumla lakini mara nyingi katika nyumba zao. Hata hivyo, uhamasishaji wa mara kwa mara wa wanawake kupitia harakati na majukwaa kama vile AFWID umeonekana kutofaulu kwelikweli na umeathiri wanaume ambao wanaumia pia. Hii ilikuwa dhahiri wakati AFWID ilikaribisha mtoto wake wa kwanza mshiriki ambaye alikuja pamoja na familia Sibanze.

Afua Wilcox-sibanze, mama, mke na mwenzake Zanele Mbeki, walihudhuria mkutano huo kwa mara ya pili, hata hivyo katika hafla hii alikuwa familia yake iliandamana naye. Alisema kuwa amekuwa akitarajia mkutano huo kwani ni mahali panapofaa kwake, lakini ilikuwa changamoto kwa sababu alikuwa amejifungua tu. Kulingana na kanuni za kijamii, mara nyingi akina mama wanatarajiwa kuhangaikia mapendezi ya wanao badala ya wao wenyewe. Hadi leo, nchi kama Sudan Kusini, Chad na Somalia hazichukulii kwa uzito mahitaji na haki za wanawake, wanawake hawana sauti halisi. Wilcox-Sibanze, anayetoka Ufalme wa Eswatini, anasema alihudhuria hasa kwa sababu ya utayari wa mumewe kumuunga mkono. Alielezea jinsi mkutano huu umemwathiri kwa njia chanya katika afya yake ya akili ambayo ilimwezesha kuongeza upendo zaidi kwa familia yake.

"Kama mwanaume, naamini kuwazuia wanawake kumezuia nusu ya uwezo wa bara." Hayo ni maneno ya Thamsanqa Sibanze, ambaye ana miradi ya kibinafsi mbalimbali inayozingatia kuinua wanawake. Anaamini kuwa majukwaa kama haya ni muhimu kwani yanawaruhusu wanawake wa bara letu kukua kama watu binafsi ambayo itawawezesha kutajirisha na kulisha vizazi vijavyo. Baba wa Iminathi Sibanze anasema aliona ni muhimu kuacha mabo yake mwenyewe ili kumpa mkewe msaada unaohitajika kwa sababu lengo kuu ni kuwa na muundo mzuri wa familia. Pia anatarajia kushirikiana na wengine kueneza maadiliko katika bara zima, kuleta mabadiliko na kufanyiza njia tofauti za utendaji. Sibanze anasema kuwa msaada kwa wanawake umekuwa haba barani, na wanawake wengi bado wanakabiliana na ukandamizaji mkubwa. Kuwa katika nafasi ambayo inaruhusu wanawake kujieleza kumemchochea kuhamasisha wengine katika maeneo yake mwenyewe. Uhamasishaji unaweza kufanywa kupitia programu za ufikiaji, semina na hata mikutano ambayo hufundisha wanaume jinsi ya kujitokeza kwa upendo.

Bi. Wilcox-Sibanze anakiri kwamba ni vigumu zaidi kuhudhuria mkutano huo ukiwa na mtoto mchanga. Anasema, "Siwezi kujihusisha kikamilifu kama kawaida yangu kwa sababu nina mtoto pamoja nami," hata hivyo bado anaweza kupata mambo makuu ya vipindi ingawa hawezi kuhudhuria zote.

# KUTAMANI KUPATA MAKAO

NA GUGULETHU MAYISELA

*"Kutamani-hisia ya hamu kubwa ya kitu."*

Katika bara lililojaa machafuko ya kisiasa na mizozo, uhamiaji mara nyingi unakuwa lazima.

Afrika ina historia ya uhamiaji yenye kuhuzunisha sana, na ilianza na uhamisho wa mababu zetu wakiwa watumwa hadi nchi za mbali. Leo, suala la uhamishaji linaendelea kuzidishwa na viongozi ambao wanashindwa kukidhi mahitaji ya watu wao, na kuchangia shida ya uhamiaji ulimwenguni. Neno "mhamiaji asiye na hati" mara nyingi huleta akilini picha ya mwanamke na mtoto wa Kiafrika, kikumbusho cha mapambano yanayoendelea ambayo wengi wanakabili. Uhamiaji ni sehemu ya hadithi ya Afrika, hadithi iliyoundwa kupitia changamoto kali na uthabiti.

Leo, kwa wengi, kuacha nchi yao kunachochewa na hali mbaya ya vita na kutokuwa na utulivu. Walakini, kwa wengine, uamuzi wa kuhama kutoka nchi moja kwenda nyingine unachochewa na kutafuta fursa bora za kazi na mustakabali mzuri.

Uhamiaji hufanya watu wajawe na kiwewe cha kihemko na kisaikolojia, kutoka kwa changamoto za kupata usajili hadi kukabiliwa na chuki dhidi ya wageni na mapambano ya kupata makao mwafaka. Kwa kuongezeka kwa uhamiaji, wengi hutamani kupata mazingira ya nyumbani na kukubalika walikohamia. Kwa mfano, kuna watu waliozaliwa na kulelewa nchini Afrika Kusini lakini serikali bado inawaona kama wahamiaji, na huwanyima utambuzi na mali wanayostahili.

Huku Dkt. Nkosazana Dlamini Zuma na wengine wakikazia miradi ya kipaumbele ya Ajenda 63 kwa ajili ya mabadiliko ndani ya bara la Afrika, pasipoti ya umoja wa Afrika uhuru wa usafiri ni moja ya miradi ya kipaumbele ambayo lazima ichunguzwe kufikia 2063.

Usafiri huru na makazi ya watu ni suala gumu, haswa katika nchi zinazokabiliwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe kama DRC, Msumbiji, Sudan Kusini, na zingine. Katika maeneo haya, watu hukimbia kiwewe cha mizozo ili kutafuta fursa salama na bora mahali pengine. Kama vile wakati wa kutembelea nyumba ya jirani, ambapo daima kuna mipaka fulani, wale wanaohamia Afrika Kusini kutafuta usalama na utulivu mara nyingi hukabili na mipaka ya uhuru wao.

Hata hivyo, mara tu amani itakapoenea kote Afrika, ni watu wachache tu watakaohisi wamehamishwa ndani ya bara. Mkataba wa Umoja wa Afrika wa 2018 wa uliopitisha Itifaki wa Uhuru wa Watu (FMP) unaahidi kuboresha hali hii, kukiwa na uwezekano wa uhuru zaidi na fursa kwa raia kote katika bara la Afrika.







# WAJASIRIAMALI WANAWAKE BOMBA WAONYESHA UFUNDI WAO KATIKA SOKO LA AFWID 2025

NA THOMAS LETHOBA









jambo kuu katika mkutano wa Mjadala wa Wanawake wa Afrika (AfWID) 2025 unaofanyika Johannesburg ni kuhusiana na ujasiriamali na ubunifu wa wanawake wanaofanyiza mabadiliko kote Afrika.

Hafla ya mwaka huu inaangazia uwezo, na katika vikao vya jumla na vya kujitenga, soko kuu huleta pamoja wanawake kutoka pembe zote za bara wakionyesha bidhaa zao. Kutoka kwa vikapu vilivyofumwa kwa mikono na seti za kipekee za nguo zilizotengenezwa kwa mikono hadi ngozi laini, soko linawakilisha dhamira ya mkutano: "Sauti ya wanawake na Uwezo kama Mawakala wa Mabadiliko."

Miongoni mwa wanawake wengi wenye ushawishi wanaoonyesha ufundi wao sokoni ni Ida Flore Maroundou, mjasiriamali aliyetajika wa miaka 37 na mtetezi mwenye wa haki za wanawake.

Kutoka Gambia, Ida yuko na majukumu chungu nzima, kama mbuni na kama mjasiriamali. Yeye ndiye mbuni wa nguo maalum, na amebuni na kutengeneza kila kipande kwa mkono, akichanganya mbinu za kitamaduni na mitindo ya kisasa.

Zaidi ya kuuza mavazi yake, Ida pia huuza vinyago zinazogusa hisia za kitamaduni na kijamii nchini Gambia. Anasema vinyago vyake huonyesha urithi wa Kiafrika, maadili, mapambano, na mafanikio ya wanawake.

"Kila kinyago ninachounda ni zaidi ya sanaa tu; ni uwakilishi wa urithi wetu wa Kiafrika, maadili yetu, na safari yenye nguvu ya wanawake leo. Kazi yangu inasimulia hadithi za ushindi wetu, mapambano yetu, na nguvu inayotusukuna ndani yetu kila siku, " Anasema Ida.

Alianza kazi yake ya kitaaluma katika kampuni ya Simu na Gabon Télécom, baadaye akahamia shirika la kimataifa kama meneja wa QHSE. Hata hivyo, shauku yake ya mabadiliko ya kijamii ilimwongoza mnamo 2020 kuwa mwanzilishi wa shirika lisilo la serikari Aurore.

Kupitia shirika lake, Ida amekuwa kiungo muhimu katika kampeni ya Wanawake wa UM ya Action Coalitions within the Generation Equality. Utetezi wake unakazia masuala muhimu kama vile vurugu za kijinsia, haki ya kiuchumi, haki ya hali ya hewa, na kukuza uongozi wa wanawake.

Mjasiriamali mwingine wa anayetambuliwa sokoni ni Zeineb Tahri Dhabbi kutoka Tunisia, ambaye huangazia kipekee mitindo ya kitamaduni na ya kisasa. Zeineb ni mtaalamu wa mikoba na viatu vilivyotengenezwa kwa mikono, kila kimoja kikiwa na miundo mingi. Ubunifu wake ni bora, una mifumo ya kipekee, na unatokeza kumbukumbu la pekee la kibinfsi.

Akifikiria juu ya mkutano wa AfWID 2025, Zeineb anasema, " tukio hili limekuwa tukio la pekee la kunifungua macho. Ninatiwa moyo kuona wanawake wajasiriamali hapa wanaoandaa huduma na nishatie. Ninahisi kuwezeshwa katika ushirikiano ambapo tunaweza kushiriki hadithi zetu, tujifunze kutoka kwa kila mmoja, na kusherehekea kazi yetu." Uwepo mwingine wenye nguvu katika AfWID 2025 ni mjasiriamali kutoka Niger, Amoussou Araoye Helene Flore, ambaye anachanganya utamaduni na mitindo kupitia vikuku vyake vilivyotengenezwa kwa mikono na viatu vya kitamaduni vya kitamaduni. Kwa uhusianisha kina cha urithi wake, yeye hutengeneza kila kipande ili akionyesha ubora na historia ya Niger.

Hapo awali alifanya kazi katika sekta ya anga-kazi zinazotawaliwa na wanaume—alisukumwa na kuangazia njia mpya na kumiiki biashara. Anaeleza, "Kuwa katika sekta ya anga, mara nyingi nilikuwa mwanamke pekee katika chumba. Uzoefu huu ulinisukuma si kuonyesha taalumu zake tu bali pia uwezo wangu wa kufanikiwa maishani. Ilinihamasisha kujitosa katika biashara yangu mwenyewe na kuunda kitu kinachoonyesha mizizi yangu huku nikiwawezesha wanawake wengine katika mchakato huo."









# MANENO YA HEKIMA: SARAH LONGWE

## NA AKHONA VALASHIYA

Mwanaharakati mkongwe wa kike wa AfWIDian kutoka Zambia, Sarah Longwe alishiriki maneno yake ya hekima na wanawake wachanga wa Kiafrika juu ya mada ya ufeministi na usawa. Alipoulizwa ni ushauri gani angewapa wanawake vijana leo ambao unaweza kusaidia kuwapeleka wanawake wa Kiafrika mbele, alisema: "Ustahimilivu, imani na maandamano." "Aluta continua kwa sababu ni lazima kuwe na usawa wa kijinsia". Mkongwe huyo anasema nywele zake nyekundu ni ishara ya imani yake na si kauli ya mtindo tu, " nywele zangu nyekundu si za mtindo, upinzani dhidi ya chuki na ubaguzi wa aina zote," alisema.

Longwe ameunda njia ya kuchanganua masuala ya jinsia kupitia Mfumo wake unaoitwa Longwe Women's Empowerment Framework. Ametumia mfumo huu katika ushauri wake mwingi uliofanywa na maidara ya jinsia katika nchi za Afrika, mashirika ya maendeleo na mashirika ya asasi za kiraia juu ya jinsi ya kutambua na kushughulikia maswala ya kijinsia ili kuwezesha maendeleo ya wanawake.

Katika maneno yake ya mwisho alisema wasichana wadogo na wanawake wadogo wanahitaji kutambua hadhi zao wenyewe na kuishi kwa ajili yazo, kupinga chuki na kuendelea kupigania usawa na furaha.



# JUMBE ZA KUUNGA MKONO KUTOKA DJIBOUTI

## NA PFARELO MUTHIGE

Wanawake wa Kiafrika wana jukumu muhimu katika kuunda mustakabali wa bara, na ni muhimu kuwawezesha ili kufikia ushawishi wa kudumu na ustawi. Ili kuinua Afrika mahali panapofaa kwenye ngazi ya kimataifa, lazima wanawake wape kipaumbele elimu na maendeleo ya taaluma. Upatikanaji wa elimu bora huwawezesha kuwa viongozi katika sekta mbalimbali, kutoka siasa hadi ujasiriamali, kukuza uvumbuzi na kuendesha ukuaji wa uchumi.

Kwa kuongezea, wanawake wa Kiafrika wanahitaji kushiriki kikamilifu katika michakato ya uongozi na maamuzi. Kwa kushiriki katika utawala na uundaji wa sera, wanaweza kutetea sheria na mipango inayounga mkono usawa wa kijinsia na haki ya kijamii. Kujenga mitandao thabiti na ushirikiano kati ya wanawake kote bara kunaweza kukuza sauti zao na kuunda umoja unaotokeza mabadiliko.

Uwezeshaji wa kiuchumi pia ni muhimu. Lazima wanawake lazima wawe na ufikiaji wa rasilimali za kifedha, masoko, na teknolojia ya kuanza na kukuza biashara. Kusaidia biashara zinazoongozwa na wanawake kunaweza kutokeza ajira na maendeleo endelevu.

Hatimaye, lazima mitazamo ya kitamaduni ibadilike ili kutambua na kuthamini michango ya wanawake. Kufanyiza programu zinazotambulisha viongozi na wavumbuzi wa kika kunaweza kuhamasisha vizazi vijavyo. Kwa kuwekeza katika elimu, uongozi, fursa za kiuchumi, na mabadiliko ya kitamaduni, wanawake wa Kiafrika wanaweza kuendesha bara kuelekea mustakabali wa ushawishi na ustawi.

**- Neima Ben Chek**












Kwa wanawake wote wa Kiafrika, tunasimama kindete katika nguvu zetu na uthabiti. Nyingi ndiyo gurudumu la bara hili, na sauti zenu ni vyombo vyenye nguvu ya mabadiliko. Tunapopitia changamoto zilizo mbele, tukumbuke: "Kwa pamoja, tunainuka; kwa pamoja, tunastawi."

Ni wakati wa kuimarisha nguvu zetu za pamoja na kuchukua hatua kwa ujasiri. Lazima tutetee haki zetu, kuhakikisha upatikanaji sawa wa elimu, huduma za afya, na fursa za kiuchumi. Acheni tusaidiane katika ujasiriamali, kuunda mitandao inayoinua na kuwezesha, na kushiriki katika uongozi wa jamii, ambapo ufahamu wetu unaweza kuunda sera zinazolenga mahitaji na matarajio yetu.

Zaidi ya hayo, acheni tutetee mazingira, na tulinde maliasili zetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Kwa kukuza mazoea endelevu, tunaweza kuhakikisha kwamba Afrika haiendelei tu, bali inastawi.

Pamoja, tunaweza kufanyiza upya hadithi ya bara letu, kuonyesha hekima na uwezo wa wanawake wa Kiafrika kwenye ngazi za kimataifa. Acheni tuinuke, acheni tuchukue hatua, na acheni tuongoze. Wakati wa mabadiliko ni sasa, na ni kazi yetu kuunda siku za usoni. Katika mshikamano na nguvu, tutaiinua Afrika hadi mahali pake panapofaa pa ushawishi na ustawi.

**- Sabira Ibrahim**

# “KUIMARISHA SAUTI: KUONGEZEKA KWA HARAKATI ZA WANAWAKE WA KIAFRIKA ILI KUUNDA SIKU ZIJAZO”

NA PFARELO MUTHIGE

*Mazungumzo Kuhusu Harakati za Wanawake wa Kiafrika: Je, Harakati za Wanawake wa Kiafrika Zina Kusudi?*



Harakati ya Wanawake wa Kiafrika ni yenye nguvu zinazoboresha mandhari ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii kote barani. Kuanzia kupigania uhuru na demokrasia hadi kutetea usawa wa kijinsia na haki za binadamu, wanawake wa Kiafrika wamekuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko yanayofaa. Makala hii inachanganua changamoto zinazokabili Harakati za Wanawake wa Kiafrika, mapendekezo ya kuziimarisha, na ikiwa zina kusudi.

Harakati ya Wanawake wa Afrika imepiga hatua kubwa kwa miaka mingi katika kutetea usawa wa kijinsia, haki za wanawake, na haki ya kijamii. Hata hivyo changamoto kadhaa zinaendelea kuzuia ufanisi na ukuaji wake. Baadhi ya changamoto nyeti ni pamoja na:

- Jamii nyingi za Kiafrika zinaendelea kuongozwa na mfumo wa ubaba, na mila na imani za jadi zinazozuia wanawake kushiriki katika uongozi, elimu, na mambo ya kiuchumi.
- Mishahara iliyopunguzwa kwa wanawake na ubaguzi wa ajira hupunguza uhuru wao wa kifedha.
- Kuondoa uhalali wa mifumo ya maarifa ya asili: Nchi za Magharibi hazitambui ujuzi unaoenziwa na wanawake wa Kiafrika, na hazielewi athari ya dawa zao katika miili ya Kiafrika.
- Viwango vya juu vya jeuri ya nyumbani, unyanyasaji wa kingono, na biashara ya kuuza watu hutishia usalama wa wanawake.
- Tofauti za jinsia katika elimu zinaendelea, huku wasichana wengi wakiacha shule kwa sababu ya ndoa za mapema, ujauzito, au ukosefu wa fedha.

Ufanisi wa harakati za Wanawake wa Kiafrika unategemea jinsi tunavyofafanua “usawa wake wenye kusudi.” Ikiwa wanawake wanaona kwamba wamefikia malengo yake ya usawa wa kijinsia, uwakilishi wa kisiasa, uwezeshaji wa kiuchumi, na haki ya kijamii; basi harakati hiyo imepiga hatua kubwa, na imefanikiwa katika nyanja nyingi, lakini bado inakabiliwa na changamoto kubwa.

Ili kuwa “sawa kwa kusudi”, inahitaji msaada mkubwa wa taasisi, ufadhili bora, na mikakati zaidi ya umoja kote barani. Inaboreka lakini badockuna kazi kubwa ili kufikia usawa wa kweli wa kijinsia.

Harakati wa Wanawake wa Kiafrika zimepiga hatua kubwa katika kupigania usawa na haki. Ingawa changamoto zinaendelea, uthabiti na uanaharakati wa wanawake wa Kiafrika unaendelea kuhamasisha mabadiliko. Kwa kufanya kazi pamoja, wanawake kote barani wanaweza kuunda siku zijazo ambapo usawa wa kijinsia utakuwa halisi zaidi na jambo hakika.





# MUHTASARI: KUFIKIRIA UPYA MUSTAKABALI ZAIDI YA BEIJING

## NA LINDOKUHLE MAINDY MABENA

### Wakili Thando Gumede

Mwanasheria Thando Gumede anajiona kama raia wa ulimwengu huu na kama kiumbe wa kiroho, na sheria kama vazi la juu tu. Kitaaluma, yeye ni wakili wa Mahakama kuu ya Afrika Kusini na mhadhiri wa Sheria na Haki za Binadamu. Anatumia taaluma yake kupambana na ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa kijinsia, ukoloni wa watu weusi, na ujenzi wa bara la Afrika. Yeye pia ni mwanzilishi wa maabara ya matibabu ya kibinafsi Nchini Afrika Kusini, iliyojitolea kuandaa huduma ya afya ya hali ya juu kwa vikundi vilivyotengwa, haswa wanawake, watu wa jinsia tofauti na LGBTQIA+, na jamii Nyeusi.

Zaidi ya hayo, pia yeye ndiye mchanga zaidi katika Tume ya Usawa wa Kijinsia Nchini Afrika Kusini, aliyechaguliwa na Rais. Hata hivyo, yeye huona hilo kuwa cheo tu, kwa kuwa katika kiini chake, yeye hujitambulisha kuwa mponyaji—wito wake wa kweli, uliopewa kimungu. Gumede huandaa uponyaji kupitia kuimarisha fahamu, kutatua matatizo, na uumbaji.




### Ni nini hukuchochea kuchukua hatua?

"Ni nini kinachonisukuma na kunihamasisha? Inafafanuliwa na neno la kiarabu Ibadah, ambayo inamaanisha utii wa kimungu. Niko hapa nikiwa na dhamira ya kujitiisha kabisa kwa mapenzi ya kimungu. Niliumbwa kupigana, kutumika kama askari wa miguu—na kuongoza, na ndivyo nitakavyofanya, bila kujali vizuizi ambavyo mfumo wa ubaba unaweza kuweka. Nimekuwa nikijiandaa kwa ajili ya wakati huu. Kila wakati ninapozungumza na kuelimisha, ninafafanua maana ya ufeministi kwangu. Ufeministi, kwangu, ni harakati isiyoyumba, inayozingatia kabisa usawa kati ya wanadamu wote, bila kujali tofauti zao ndogondogo."



### Michal Petros


Michal Petros, mpiga picha na meneja wa mradi aliyejitolea kujenga jamii, ni Mmarekani wa Eritrea. Yeye hujitambulisha kama mwandishi wa hadithi, na historia ya kitaaluma katika Masuala ya Kimataifa, akizingatia utambulisho na utawala Barani Afrika. Kazi yake imejikita katika kukusanya fedha na maendeleo kwa mashirika yasiyo ya faida, na amefanya kazi na kuishi Nchini Kenya, Eswatini, na Algeria. Mapenzi yake kwa haki za binadamu yanatokana na urithi wake wa Eritrea.

Eritrea ilipata uhuru mwaka wa 1991, na Michal alizaliwa mwaka wa 1997. "Leo, tulizungumza juu ya kuheshimu wazee wetu, na kile kinachovunja moyo wangu ni kwamba wale waliopigania uhuru wetu hawajawahi kujua Eritrea huru. Tangu 1991, nchi yetu imebaki chini ya udikteta, na tangu 2001, hakujakuwa na uhuru wa vyombo vya habari—bila shaka hata kabla ya hapo, lakini kisheria tangu 2001. Kuna kulazimishwa kuandikishwa jeshini kitaifa, kutia ndani wanawake vijana, na makumi ya maelfu kukimbia kila mwezi, hasa kutoroka kuandikishwa jeshini ili wakatafute elimu na maisha nje ya mipaka ya Eritrea."

### Ni nini hukuchochea kuchukua hatua?

"Kama mwanachama wa diaspora, ninasema siwezi kurudi Eritrea. Hata hivyo, nimejitolea sana kuleta mabadiliko nikiwa diaspora, kusaidia wale ambao wanatekeleza mageuzi na kuwasaidia wale wanaokimbia nchi hiyo. Kazi nyingi katika diaspora inazingatia makazi mapya ya wakimbizi, na sasa tuna kizazi kipya cha Waeritrea ambao wanaweza kujitetea wenyewe—wale ambao wamepatia udikteta moja kwa moja. Tunafanya kazi pamoja nao ili kupaaza sauti zao. Kama Mmarekani wa Eritrea, ninatambua vile nimebarikiwa, na nitatumia baraka hizo kuinua wale wanaovumilia ukandamizaji nyumbani."

# KAULI YA WANAWAKE WA SUDAN KATIKA MKUTANO WA AFWID



Muwe na amani ninyi washiriki waheshimiwa wa Mkutano wa Mjadala Wanawake wa Kiafrika.

**Pokeeni Salamu na Heshima.**

Ni furaha yetu kukutana na ninyi hapa ili kujadili masuala ya uwezeshaji wa wanawake Barani Afrika katika nyanja zote za usalama, amani, afya, na uwezeshaji wa kiuchumi. Hata hivyo, tunakuja kwenye mkutano huu tukiwa na maumivu mengi yanayotokana na mateso ya muda mrefu kwa wanawake wa Sudan kufuatia vita vinavyosababisha maumivu kwetu sote.

Vita hivi vinavyoendelea, wanawake wa Sudan wamekabiliwa na aina mbalimbali za udhalilishaji, ikiwa ni pamoja na ubakaji, kuhamishwa kwa nguvu, utumwa, na kulazimishwa kubadilishana chakula na ngono, ikisababisha kuwa na mamilioni ya wakimbizi wanawake, pamoja na kupoteza msaada. Vita vya sasa hasa vinalenga wanawake, na zaidi ya hili Sudan inakabiliwa na njaa kali iliyoelezwa na ripoti za Umoja wa Mataifa kuwa mbaya zaidi duniani, ikiathiri zaidi ya Wasudi milioni 26. Licha ya hayo, kuna matatizo makubwa ya kuandaa misaada ya kibinadamu kwa wanaohitaji, kuzuka kwa magonjwa ya kuambukiza, huku wenyeji wakizuiwa kuchangamana kwa vyovyote na jamii ya kimataifa.

Wanaume na wanawake wa Sudan, waliopo na waliohama, wanakabiliwa na hali mbaya na ngumu sana, na tukiwa wanawake wa Sudan hapa, tunawaomba mjiunge nasi kudai hitimisho la vita na kwamba kila mtu afanye kazi na sisi ili kurejesha usalama, amani, na upatikanaji wa chakula. Pia tunataka kauli hii ifikie Serikali zote za Afrika, Umoja wa Afrika, Baraza la Amani la Afrika, IGAD, na mashirika yote ya Umoja wa Mataifa, pamoja na washirika wengine wa kimataifa ulimwenguni. Tunajua kwamba wanawake ndio walioathiriwa zaidi na vita, na pia tunaamini kwamba wanashikilia ni nguzo kuu ya amani.

Tunatuma shukrani zetu za dhati kwa waandaaji wa mkutano huu kwa kutupatia fursa hii ya kuibua masuala ya wanawake Nchini Sudan wakati huu muhimu, na kupaza sauti zetu kukomesha vita na kumaliza mateso ya mamilioni ya Wasudi hasa wanawake, watoto, wazee, walemavu nk.

**Wajumbe Wanawake wa Sudan**
**Januari 29, 2025, Johannesburg**

# AMANI ITALETWA NA NINI AFRIKA?

## NA JODI A. LAWRENCE

Kwa sasa, kuna mapigano 35 yanayoendelea Barani Afrika, yanayoathiri maeneo kama vile Misri, Libya, Morocco, Sahara Magharibi, Burkina Faso, Somalia, Sudan, na Sudan Kusini.

Ni jambo linalohangaisha sana kwamba mapambano hayo mengi yanachangiwa na uvutano wa mataifa ya magharibi, kutia ndani Marekani, Ufaransa, na Urusi. Kuhusu Sudan Kusini, jukumu la Falme za Kiarabu katika vita vya wenyewe kwa wenyewe haliwezi kupuuzwa.

Kama ilivyo na vita vyote, wanawake na watoto hubeba mzigo mkubwa zaidi, wakifa wengi zaidi na kufanyiza idadi kubwa zaidi ya wakimbizi. Mwaka huu, katika mkutano wa Mjadala wa Wanawake wa Afrika (AfWID), wanawake wameelezea majonzi walio nayo kwa nchi zao na familia zao zilizoathiriwa na vita. Wajumbe wengi wamezungumza juu ya ukosefu wa mshikamano kati ya wanawake kote barani, wakisisitiza kushindwa kwa wanawake kutambua migogoro inayoendelea na kupinga viongozi wanaofaidika na vita.

Dkt. Zoneziwoh Mbondgulo alizungumza kwa ufasaha kuelekea United Nations Security Council Resolution 1325, ambalo linatambua athari za vita kwa wanawake na linataka ushiriki wao sawa katika kufanya maamuzi ya amani na usalama. Alibainisha kuwa wakati maadhimisho ya miaka 25 ya azimio hili yanapokaribia, wanawake wengi barani Afrika, wakiwemo wale waliokuwepo kwenye mkutano huo, bado hawajaona utekelezaji wake wa maana. Azimio hilo bado halijasaidia wanawake katika maeneo yenye migogoro.





Wakati wa mjadala wa jopo, Nomboniso Gasa, akizungumza kutoka kwa wahudhuriaji, alisema kwamba wanawake mara nyingi wameendelea kutetea mifumo ya ubaba, wakati mwingine kwa hasara ya wanawake wengine. Alisema hii imechangia kunyamazisha wanawake na kuwanyima haki zao wale wanaotaka kupinga mawakala wa migogoro katika maeneo ya vita kama vile Senegal, Somalia, na Jamhuri ya Afrika ya kati.

Katika hafla hiyo, kikundi cha wanawake wanaofanya kazi kilisisitiza uhitaji wa kufikiria zaidi maisha ya baadaye ili kuvunja utamaduni wa vita vinavyoenea barani. Katika kipindi cha majadiliano, wajumbe walifikia mkataa muhimu: kuna haja ya dharura ya ujumbe wa amani unaoongozwa na wanawake katika maeneo ya migogoro na ya kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika wa wanawake, utakaoundwa kwa kufuata kigezo cha uongozi wa wanawake katika Umoja wa Mataifa.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa wanawake lazima wawe na elimu bora kuhusiana na asili ya migogoro—sio tu kama nguvu inayowaathiri kimwili na kisaikolojia, lakini kama jambo tata la kijamii na kisiasa linalohitaji ushiriki wao. Ni lazima wanawake wahusishwe katika majadiliano ili kupata amani Barani Afrika na utatuzi wa migogoro, kama vile wanavyohusishwa katika shughuli za kila siku katika kijamii.



# MIAKA +30 BAADA YA BEIJING: WANAWAKE WA KIAFRIKA WAHAMASISHA MABADILIKO

### NA NKHENSANI NKHWASHU

Kipindi cha kujitenga ili kuzungumzia miaka +30 baada ya Beijing katika hafla ya Mjadala wa Wanawake wa Afrika (AFWID) kiliandaa nafasi ya kutathmini upya maendeleo na uwajibikaji katika ajenda ya jinsia ya Afrika, miongo mitatu baada ya mkutano wa Nne wa Dunia wa wanawake 1995 huko Beijing, China. Mkutano huo wa kihistoria, ambao ulihudhuriwa na wawakilishi kutoka nchi 189 na maelfu ya mashirika ya kiraia, ulipitisha Azimio la Beijing na Jukwaa la Utekelezaji—mfumo kamili wa kuendeleza haki za wanawake na kufikia usawa wa kijinsia ulimwenguni.

Akiwa mwanajopo, Amel Samoud Khamari, Rais wa Chama cha Tunisia cha Utawala na Fursa Sawa Kati ya Wanawake na Wanaume katika Nafasi za Kufanya Maamuzi (ATGEC), alishiriki hadithi yake kuhusu mkutano wa Beijing mnamo 1995.

“Ilikuwa mkutano mzuri sana kwangu kama mwandishi mchanga wa habari. Nilikuwa na umri wa miaka 28 tu na nilikuwa nimemwacha mtoto wangu wa miaka mitano. Ilikuwa heshima kuchaguliwa kuwa sehemu ya wajumbe waTunisia, hasa kama mwanachama mchanga zaidi katika kundi hilo.”

Khamari alieleza kuhusu msisimko wa kuona wanawake kutoka nchi mbalimbali, malezi, na dini, wote wakizungumza lugha tofauti lakini wakiwa wameunganishwa na kusudi moja. Pia alizungumza juu ya uzoefu wake kama mwanamke katika tasnia ya vyombo vya habari na jinsi alivyotumia sauti yake kupambana na umaskini na ukosefu wa usawa, pamoja na changamoto zingine.

Kikao hicho kisha kilifungua nafasi kwa wanahabari waliohudhuria, wakiwaalika washiriki maoni yao ya kibinafsi na ufahamu kuhusu ikiwa kuripoti juu ya maswala ya wanawake kumeboreka tangu mkutano wa Beijing. Ingawa iliripotiwa kwamba kumekuwa na maendeleo, wengi walionyesha wasiwasi kuhusu tofauti zinazoendelea kati ya waandishi wa habari wa kike na wa kiume, wakisisitiza mapambano yanayoendelea ya usawa ndani ya mazingira ya vyombo vya habari.

“Sekta ya vyombo vya habari bado ni ya ubaba, na ina mitazamo iliyokita mizizi. Mwandishi mmoja wa habari wa kike alisema, “Hadithi zinazochukuliwa kuwa ‘habari laini’ mara nyingi hupewa waandishi wa habari wa kike, wakati waandishi wa habari wa kiume wanapewa mada za ‘habari ngumu’ kama siasa na uchumi.”

Wahu Kaara, mwalimu mashuhuri wa Kenya, mwanaharakati, na mwanaharakati wa haki ya kijamii, alikumbuka wazi mkutano wa Beijing, akiielezea kana kwamba ulifanyika jana tu. Alizungumza juu ya shauku na azimio la wanawake walikusanyika huko, akibainisha jinsi vizuizi vya lugha havikuwahi kuzuia maono yao ya pamoja.

“Wanawake walidai nafasi za umma kwao wenyewe-hawakuwahi kukabidhiwa. Walifanya wanaloweza ili kuchukua mamlaka.”

Kaara alihimiza kwamba sasa si wakati wa maombolezo bali wa kuchukua mamlaka.

NgoN-Baba Née Noufere Céline, Mwenyekiti wa Mafubo Centrafrique, Shirika Lisilo la Kiserikali katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, alisisitiza uhitaji wa wanawake kukumbatia mabadiliko ya dijititali.

Alisisitiza kuwa teknolojia inapaswa kutumiwa kufikia wanawake katika maeneo ya vijijini, kutetea elimu na mafunzo katika ujuzi wa kidijitali ili kuwawezesha wanawake wawe mabingwa wa udijitali na kufungua uwezo wao kamili.

Wakati wote wa majadiliano ilionekana kwamba walikubaliana kwamba maendeleo makubwa yamefanywa tangu mkutano wa Beijing: lakini licha ya hatua zilizochukuliwa, kazi nyingi zinabaki. Washiriki walikubaliana kwamba jitihada na ujitoleaji wa kudumu ni muhimu ili kufanyiza mabadiliko zaidi.






# WALEZI WA ARDHI: CHANGAMOTO KUU NA MABADILIKO

NA LEBOGANG MATHEBULA









Upatikanaji wa chakula na kujitegemea zimekuwa mahangaiko ya muda mrefu kote Afrika. Licha ya mandhari kubwa ya bara na maliasili tajiri, kilimo mwafaka bado ni changamoto, haswa kwa wakulima wa kike ambao jukumu lao muhimu ni uzalishaji na usambazaji wa chakula.

Siku ya tatu ya AFWID 2025 iliandaa nafasi kwa wanawake wa Kiafrika katika kilimo kuelezea changamoto zao na kupanga mikakati ya mabadiliko. Wakiongozwa na Mercia Andrews, Mkurugenzi wa Trust for Community Outreach and Education, warsha hiyo ilileta pamoja wanawake kutoka mikoa mbalimbali kujadili vikwazo nyeti wanavyokabili. Suala kubwa lililoletwa na wanawake kutoka nchi zinazozungumza Kiarabu lilikuwa athari za migogoro ya silaha inayoendelea, inayofanya maeneo makubwa ya ardhi yasifae kwa kilimo. Nchini Sudan, vita vya wenyewe kwa wenyewe vimevuruga sana ugavi, vikisababisha uchumi kuzorota hivyo kuzidisha uhaba wa chakula.

Katika bara lote, ukosefu wa fedha uliibuka kama changamoto kubwa zaidi. Bila msaada wa kifedha, wakulima wanawake hawapati kwa urahisi rasilimali muhimu kama vile maji, mbolea, gharama, na zana za kisasa za kilimo. Zaidi pengo hili la kifedha kuzuia tija, pia linapunguza uwezo wao wa kushiriki katika utafiti, kutumia mbinu mpya za kilimo, na kushindana katika masoko ya ndani na ya kimataifa. Ulimwengu unapoendelea katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, wanawake hawa wanajikuta pambaya, kwa kushindwa kutumia teknolojia mpya katika kilimo chao.

Ukosefu wa maji huleta changamoto nyingine kubwa. Maeneo mengi ni kame hivyo kufanya iwe vigumu kulima. Tatizo kubwa la sera lilitokana na Mkataba wa Maji wa Kenya wa Mei 19, 2010, ambao ulipiga marufuku matumizi ya maji ya Mto Nile kwa ajili ya ukulima. Uamuzi huo ulileta pigo kubwa kwa kilimo endelevu. Hata hivyo, mwaka 2025, Waziri wa Maji Charity Ngilu alitangaza kwamba mataifa ya Afrika Mashariki sasa yana uhuru wa kutumia rasilimali za maji wanavyoona inafaa, akatoa matumaini mapya kwa wakulima wanaopambana.

Changamoto nyingine kubwa ni mahitaji ya kutokomeza vyakula vilivyozalishwa kwa kemikali (GMOs) na uhifadhi wa kilimo asili. Wakulima wengi wa Kiafrika wanaamini kwamba mbegu zao za asili zina dawa, zina lishe bora, na zimeunganishwa sana na utambulisho wao wa kitamaduni na kiroho. Mary Sakala wa Zambia alieleza kwa shauku msimamo huu: "Chakula tunachokula ni sehemu ya utambulisho wetu. Mbegu zetu za asili zinaweza kuwa dawa, zinaweza kuwa chakula, na zinaweza kutuunganisha kiroho." Ingawa Shirika la Chakula na Dawa (FDA) linasema kwamba chakula cha GMO hakina hatari yoyote kiafya, uchunguzi mbalimbali wa kibinafsi unaonyesha kwamba miongoni mwa wakulima Waafrika hilo si kweli.

Pamoja na changamoto hizi, wito wa ufadhili ili kuwa na mabadiliko ya hali ya hewa ni wa dharura, haswa kwa wanawake wa mashabani ambao mara nyingi huitwa kuwa wakulima wadogo. Roseline Orwa wa Kenya alisisitiza haja ya wanawake kuungana na kudai msaada wa kifedha ili kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwenye kilimo.

Licha ya matatizo mengi yaliyozungumziwa, wanawake hao waliondoka kwenye mkutano huo wakiwa na azimio jipya. Sauti yao ya pamoja na kujitolea bila kuyumba kwa mabadiliko kunaashiria harakati yenye nguvu ya mageuzi ya sera na kuongezeka kwa utetezi wa kilimo endelevu. Wanawake hawa sio tu walezi wa ardhi; wao ni wasanifu wa siku zijazo ambapo usalama wa chakula ni ukweli kwa wote.

# AFWID KUCHUKUA MAONI KWENYE REDIO YA SAFM




## Mustakabali tunaotaka-mustakabali uliojengwa kwa wanawake Wa Kiafrika na wanawake Wa Kiafrika.

AfWID ilichukua mawimbi ya REDIO YA SAFM siku ya pili Wakati Taweni Gondwe Xaba aliandaa programu ya uongozi wa mawazo ya Kutafuta Maoni.

Kwenye jopo hilo, alijiunga Na Mwanachama Wa Nana Magomola – Wdb Trust, Mwanachama Wa Kamati Ya Uongozi Ya Emma Kaliya – AfWID Na Mratibu Wa AFWID SADC, Saida Ali – Afwid Mratibu Wa Afrika Mashariki, Na Sara Longwe – Beijing Mkongwe Wa 1995, na katika wasikilizaji walikuwa wanawake kutoka pembe mbalimbali za bara letu tajiri na nzuri.

Majadiliano yenye nguvu na ya kusisimua ya saa moja yalilenga mada Ya AfWID ya Kujenga kuelekea siku zijazo tunazotaka, Na Wanawake Wa Kiafrika Kwa Wanawake Wa Kiafrika.

Washiriki wa jopo walipima jukumu ambalo wanawake wanahitaji kuchukua hatua ili kukabiliana na changamoto zinazokabili bara kuhusu amani na utulivu, ulinzi wa rasilimali,kuwasaidia vijana na kuwa mstari wa mbele katika kutengeneza sera, na ukuaji wa uchumi na pia katika mada zingine kubwa.

Hatua muhimu za kihistoria kutoka mikutano ya wanawake ya zamani ziliangaziwa, pamoja na maendeleo ya mifumo kama Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake. Mazungumzo hayo yalikazia uhitaji wa suluhisho zinazoweza kutekelezwa,kuandaa fedha kwa miradi inayoongozwa na wanawake, na kuondoa vizuizi kwa wanawake vijana kuchukua majukumu ya uongozi. Changamoto, kama utawala usio na utulivu katika baadhi ya mikoa, zilikubaliwa kama vikwazo vya maendeleo. Kulikuwa na wito wa umoja, kujitegemea, mipango ya kuokoa jamii, na sera za kuendelea kuimarisha haki za wananawake na kusonga kimaendeleo.

## Nana Magomola, Mwanachama Wa Wdb Trust

Wazo hili lilikuwa la kuleta pamoja wanawake kutoka nchi 55 kuwa na mazungumzo haya muhimu, ilionekana kuwa jambo kubwa lakini la kusisimua. Tulijua ni mada ambayo tulihitaji kuunga mkono. Jukwaa hili linaturuhusu kuwasidia wanawake kujieleza na kuwapa uwezo katika kuleta suluhisho. Kwa sisi, ilikuwa juu ya kuhakikisha wanawake kutoka kila aina ya maisha, pamoja na wale walio katika maeneo ya vijijini na walio katika meneo ya mashambani, wanaweza kuwa sehemu ya mazungumzo haya.

## Saida Ali

Tunahitaji matendo yanayoweza kutekelezwa. Wanawake hapa wanashiriki mikakati inayoweza kufaulu na kuonyesha roho ya uongozi. Wengi wao wamesaidia pakubwa katika jamii zao, hasa wanawake vijana. Kwa mfano, wanawake vijana Kutoka Sudan Kusini na mikoa mingine wamejitolea kurudi nyumbani na kujipanga. Wanachukua majukumu ya uongozi na kudhibitisha kuwa hauhitaji elimu rasmi au utajiri ili kuongoza. Hii ni fursa nzuri kwa wanawake wote kujifunza na kukua.

## Sara Longwe


Safari ilianza na mikutano ya awali, ikiwa ni pamoja na mkutano wa Beijing wa 1995, ambao uliunda "Jukwaa la Beijing la Utekelezaji." Hati hii iliweka msingi wa kuendeleza haki za wanawake duniani kote. Mikutano ya Wanawake wa Afrika ulitimiza jukumu muhimu katika kuunda nyanja kuu za kukazia, pamoja na umaskini, elimu, vurugu dhidi ya wanawake, na uwezeshaji wa kiuchumi. Masuala haya bado ni muhimu katika ajenda yetu. Kwa miaka mingi, tumeona nchi nyingi zikiridhia makubaliano, lakini changamoto imekuwa kutekeleza maazimio hayo.

## Emma Kaliya

Azimio 1325 lilianzishwa ili kuhakikisha uwakilishi wa 30% wa wanawake katika serikali, lakini hakuna nchi ambayo imefikia azimio hili. Huenda hii ndiyo sababu mizozo inaendelea kuibuka hata baada ya juhudi za kuikandamiza. Kufanya maamuzi ni muhimu, na wanawake lazima washirikishwe. Mara nyingi, kutokuwepo kwao katika majadiliano ya amani kunadhoofisha maendeleo. Bila wanawake, mchakato haukamiliki, na amani endelevu haipatikani.

> *Ni kuhusu kuunda mifumo ya utetezi endelevu. Tunahitaji kuhakikisha sauti za wanawake zinasikika katika kila ngazi ya kufanya maamuzi. Kwa mfano, microfinance imebadilikana sana katika maeneo mengi, lakini lazima pia tufikirie zaidi ya "micro" na kulenga miradi mikubwa inayofaidi jamii nzima.*



# MIMI NDIYE YULE AFRIKA IMEKUWA IKISUBIRI

## Ahadi za kibinafsi za Kuendeleza Ajenda ya AfWID

Ninatambua kuwa taasisi ni muhimu, lakini ufanisi wao unategemea wakala wangu kibinafsi kuendesha mabadiliko na kushirikisha nafasi zangu. Utetezi wangu kwa wanawake wa Kiafrika ni kwa msingi wa upendo na kujikubali, na ninaushiriki kwanza na familia yangu mwenyewe, kisha nanaupanua kwa jamii yangu. Ninajitolea kuelezea na kusaidia wanawake wa Kiafrika kokote ninapoweza, kupitia hatua ninazochukua, maneno ninayozungumza, na nafasi ninazoshiriki. Nikiwa mshiriki wa mkutano huu, ninajitolea kuendeleza ajenda ya AfWID kupitia:

1. **Uwezeshaji Kupitia Maarifa:** Ninajitolea kutafuta kikamilifu habari za kuaminika, zilizothibitishwa, kuendelea elimu kuhusu Harakati za Wanawake wa Kiafrika na kushiriki mambo hayo kwa uwajibikaji. Ninaelewa kuwa uwezo wetu wa pamoja ni kufuatia kusema ukweli na kupaaza sauti ya wanawake, na nitaweka kipaumbele usambazaji wa habari iliyothibitishwa, inayofaa kuwawezesha wanawake katika jamii yangu.

2. **Uponyaji na Kutambua Kiwewe:** Ninakubali kwamba sisi sote tunabeba kiwewe cha kizazi, na ni lazima kwanza tushughulikie maumivu haya ikiwa tutafanikiwa. Ninajitolea kusaidia michakato ya uponyaji, kuelewa kuwa mabadiliko ya kweli huanza na mtu binafsi kisha kushirikisha wengine. Nitakuza mazingira ambapo wanawake wanaweza kushiriki uzoefu wao kwa usalama, na ambapo ushirikishi ni sehemu ya mjadala na uharakati wangu.

3. **Utetezi wa Wanawake Waliohamishwa:** Nitawatetea wanawake waliohamishwa, haswa wale walioathiriwa na uhamiaji, kuhakikisha wanapata rasilimali, haki, na msaada wanaohitaji. Nitaunda nafasi ya wao kusikilizwa na nitafanya kazi ili kuondoa vizuizi vya uhuru na fursa zao. Msingi wa utetezi wangu utakuwa katika kutambua heshima yao ya asili, na nitapigania uwezeshaji wao kwa hali na mali.

4. **Mshikamano na Uwajibikaji Binafsi:** Ninajitolea kufikiria "mwanamke kwanza" katika chochote ninachofanya. Nitatenda kwa mshikamano na wanawake wa Kiafrika katika kusaidiana kabisa. Sitasubiri hatua za serikali lakini nitachukua jukumu la kibinafsi kufanya mabadiliko ninayotaka kuona. Mabadiliko ya pamoja huanza na matendo yangu binafsi, na nitatumia ushawishi wangu binafsi kuleta mabadiliko tunayotaka.

5. **Kutetea Amani na Mshikamano:** Nitatetea ujumuishaji wa wanawake katika kuleta amani na utatuzi wa migogoro, kuhakikisha sauti zao zinasikika katika majadiliano ya kimsingi na ya kiwango cha juu zaidi. Nitaendeleza mshikamano katika mipaka, nitasaidia wanawake wa Kiafrika katika maeneo ya migogoro, na kuhakikisha kwamba matendo yangu yanakazia amani, umoja, na maendeleo.










6. **Kuimarisha Harakati za Wanawake Afrika:** Ninajitolea kuwa mshiriki halisi katika Harakati za Wanawake wa Kiafrika, kuhakikisha inaendelea kujumuisha, ina nguvu, na inasikazia mahitaji anuwai ya wanawake wa Kiafrika. Nitaunga mkono kuundwa kwa mpango wa umoja kuhusu utetezi wa pamoja, kuimarisha sauti za wanawake katika bara zima na kutambua kwamba zaidi ya kufaidi mtu mmoja tu, harakati hiyo inalete mabadiliko kwa wote.

7. **Suluhisho Endelevu kwa Upatikanai wa Chakula:** Nitaunga mkono ushiriki wa wanawake katika kilimo endelevu na upatikanaji wa chakula, nikitetea sera zinazokazia kilimo na uongozi wa wanawake katika haki ya kiikolojia. Nitaendeleza elimu kuhusu masuala haya na kuhakikisha kwamba matendo yangu yanaonyesha kujitolea kulinda mbegu za asili, kuwawezesha wakulima wa kike, na kukuza ujasiri katika mifumo ya chakula Afrika.

8. **Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wanawake:** Nitakuza ujuzi wa kifedha na uhuru kwa wanawake wa Kiafrika, nikisaidia mipango ya kuwapa wanawake zana na rasilimali za kustawi. Nitapinga mifumo ya kiuchumi ya ubaba na nitatetea sera zinazowawezesha wanawake kiuchumi. Kujitolea kwangu binafsi kwa haki ya kiuchumi huanza nyumbani, kwa kuandaa elimu ya kiuchumi na kuhamasisha uhuru wa kiuchumi katika jamii yangu.

9. **Ulinzi na Usalama wa Wanawake:** Nitatetea sheria za kuwalinda wanawake dhidi ya unyanyasaji na nitahakikisha usalama wa wanawake unapewa kipaumbele katika maeneo ya migogoro na kwingineko. Nitawatetea waathiriwa wa kivita, na nitaandaa msaada kwa vitendo na kihisia inapohitajika. Kujitolea kwangu kulinda wanawake huanza na kuhakikisha nafasi salama katika maisha yangu na jamii.

10. **Uwezeshaji Kupitia Sauti Yangu na Mitandao:** Ninatambua zana za kutetea haki za wanawake kuwa nguvu ya sauti yangu katika mitandao. Nitatumia ushawishi wangu kupaaza sauti za wanawake wa Kiafrika, kuunga mkono mshikamano na hatua ya pamoja. Ninaelewa kuwa uongozi unatokana na uwajibikaji wa pamoja, na ninajitolea kuchukua hatua inayoendeleza usawa wa kijinsia.

Maazimio haya ya kibinafsi ni ukumbusho kwamba mabadiliko tunayozingatia yanaanza na kila mmoja wetu. Kupitia matendo yangu, ninataka kuchangia ajenda ya AfWID, nikijua kuwa juhudi za kibinafsi zikijumuishwa, zina nguvu ya kuunda mabadiliko ya kudumu. Kila hatua ninayochukua itawahamasisha wengine kufanya vivyo hivyo, na itaunda mandhari yanayoinua wanawake wa Kiafrika na kuimarisha mustakabali wetu wa pamoja.

# INACHUKUA KIJIJI

Katika kila hafla inayofanikiwa, kuna mashujaa wasioangaziwa—wanaofanya kazi bila kuchoka ili kuhakikisha kuwa kila kitu ni shwari. Katika mkutano wa AfWID wa Mwaka huu, wajitoleaji wetu walikuwa gurudumu la hafla hii. Walikuwa ndio misuli, gundi, na nishati iliyoshikilia hafla yote pamoja. Kuanzia tulipowasili, walitusalimu kwa uchangamfu na urafiki, wakipunguza hofu zetu na wakatufanya tuhisi nyumbani. Tuliwaona wakiwa wa kwanza katika uwanja wa ndege na tunawaona wakiwa wa mwisho tunapoondoka.

Katika kipindi ambacho waliozeeka wana wasiwasi wa jinsi vijana wataunda mustakabali na kuongoza bara letu, ni wazi kuwa mustakabali wa Afrika tayari uko mikononi inayofaa. Vijana wanasimamia, wakituonyesha maana ya uongozi, ujitoleaji, na huduma. Bila wajitoleaji hawa machachari, hakuna AfWID. Walijitolea kwa shauku kuliko ilivyojarajiwa, wakithibitisha kwamba wao ndio kizazi kijacho cha viongozi-na wako tayari.

Asanteni sana waliojitolea kwa muda wenu, nishati, na moyo kufanikisha tukio hili. Ninyi ni mabingwa wa kweli wa Afrika ya kesho, na tunawaona.

**Linda Vilakazi**
**Meneja wa Programu za AfWID**











# MIZIZI ILIYOKITA YA MITI INAYOOZA

## CHIGOMEZGO GONDWE, 2025

Mfumo wetu wa maisha hutabiriki
ambako wanaume ni wafalme wa mamlaka yasiyo halali,
wanaopongezwa kwa kubomoa na kujenga,
huku wanawake wakifinyiliwa kwa kimya kinyemi,
wakiadhibiwa kwa kutumia silaha ileile ya maisha.

Katika kivuli cha miti iliyooza,
tunawapatia wana wetu matunda makali ya mfumo wa ubaba,
huku tukiwaingiza katika udugu
unaoathiri thamani yao kutoka ujinga wa kiutawala.
Kizazi baada ya kizazi,
tunaendeleza uharibifu.
Wamama wa harakati,
wamenaswa kwenye mfumo,
wa kuinua wanaume wanaokaza minyororo inayowakadamiza.

Sisi,
wanaozaa watoto,
wamekuwa waanzilishi wa ukandamizaji wetu wenyewe.
Wanasema ni utamaduni, na tunabeba jukumu hilo,
lakini utamaduni ni mto unaopinda na kukua,
sio bwawa lililosimama ambako ndoto huoza.
Moto wetu, siku moja ulikuwa kizingiti,
na sasa ni moto mdogo,
unaofyonzwa na moshi wa nyumba
unaochoma kwa hasira isiyo na sauti.

Ni kioo gani kinachotuonyesha sasa,
kilichofungamanisha na mizizi hii ya miti inayooza
ambayo haikui tena,
iliyofungwa kwa vizuka vya mithali
iliyosemwa siku moja kwa usawa na fadhila?

“Mwidaji atajigamba kabisa,
hadi pale simba atapisimulia hadithi yake”
hivyo ndivyo wanasema,
lakini namna gani kuhusu simba wa kike,
ambao mgurumo wao huishia dhoruba ya kitamaduni?

Naam,
hatutadumu katika hali ya balagha tena,
tukirambaramba kama maji ya visima sumu.
Kupitia akili zetu tutakausha kabisa visima hivi,
tufanyize mito ya upinzani kwa mikono yetu,
na ze tufanyimafuriko katika nchi kame
tukiwa na ghadhabu na sauti tusiyoogopa kuinua.

Choma mizizi inayooza -
choma utupu wao katika nguzo za moto.
Acha majivu yawe mchanga wetu wenye rutuba na uthabiti.
Panda mbegu za mapinduzi kwa uwezo kamili,
wafundishe watoto wetu kutumia haki kama mapanga
yanayokata uwongo uliokithiri.

Pigania ukombozi kutoka kwa minyororo ya historia mbovu,
andika na usimulie hadithi za ushindi wetu wenyewe.
Vua udanganyifu wa ukuu na nguvu
kwa uwazi wetu wa kimaadili na Umoja.
Acha ulimwengu uonekane wazi katika siku zijazo.
Pindua ngome za ukimya wa kulazimishwa.
Bomoa mamlaka yaliyojengwa ili kutukandamiza.
Sema: ‘Nyeusi, usipasuke’ kwa sababu haturudi nyuma!’

Tunajua sisi ni nani na tunachokusudia kuwa.
Sisi ni watunzaji wa nyumba na walezi wa watoto,
wenye hekima na wasema kweli.
Mikono yetu sio tu ya kutengeneza makaa,
imechomwa na kupigwa,
hii ndiyo mikono inayoboresha mataifa.
Tunahisi kuvujika mioyo,
Maneno yetu yanadhihirisha siri zilizofishwa kwa miaka mingi,
yakiashiria siku zijazo zenye matumaini.

Sisi si tu mwanamume, mwanamke, au wao;
sisi ni wanadamu, sio viwakilishi, lebo au alama,
sisi ni wanaume au wanawake tu,
tulioumbwa kwa mfano wa Mungu Aliye Juu Zaidi.
Hatutapoteza sisi ni nani,
uwepo wetu hautafifia,
katika simulizi la kimataifa la mageuzi ya kijamii
sauti zetu zitashikilia ukweli wa wokovu.

Sisi ni gurudumu,
linaloendesha ulimwengu huru,
lenye misukomo ya siku zijazo ambayo isiyosubiri,
gurudumu la vizazi ambavyo bado havijazaliwa.
Sisi ni ushuhuda wa Ukweli na Nguvu,
zinazoonekana wazi kabisa.

Kupitia ujenzi mpya wa kitamaduni
na wa maadili,
tutafungua nyuzi zilizofungamanishwa na
tushone vazi jipya la maono yetu bora zaidi.
Lazima jana isahaulike na
Yaliyopita si ndwele.
Kwa hiyo, Black don’t crack, ‘ kwa sababu sisi haturudi nyuma!
Semeni, Black don’t crack, ’cause we are not going back!



WDB | TRUST